SUPA JACKPOT
TZS. 1,090,583,531
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Kampuni** ya DRC yatangaza filamu ya the Royal Tour

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Machi 19, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581254

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Majaliwa awawashia moto Ma-DC goigoi

UKURASA 2




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akifunga mafunzo kwa wakuu wa wilaya Tanzania Bara, kwenye Ukumbi wa Mtakatifu Gaspar jijini Dodoma, jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## CCM yacharuka makandarasi kuchelewesha miradi maendeleo

UKURASA 2

## ACT- Wazalendo yawakaba koo polisi, usalama kupotea kwa watu

UKURASA 3

MICHEZO **SIMBA YAFANYA MAUAJI AFRIKA** UK. 24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

## CCM yawacharukia makandarasi kuchelewesha miradi maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimecharuka kuhusu makandarasi kushindwa kukamilisha miradi kwa wakati na kuwataka wakuu wa mikoa kuwachukulia hatua za kisheria kwa madai kuwa wanawajengea chuki wananchi dhidi ya serikali.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Mohamed Said Mohamed, alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipohutubia wananchi waliohudhuria kwenye maadhimisho ya kitaifa ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Maadhimisho hayo ya kitaifa ya miaka miwili ya rais Samia yalifanyika mkoani Mbeya na kuwashirikisha viongozi mbalimbali wa chama na serikali kutoka katika mikoa ya nyanda za juu kusini na baadhi wa kitaifa.

Aliwataka wakuu hao wa mikoa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo ili itekelezwe kwa viwango vinavyoendana na thamani halisi ya fedha zinazotolewa ili kuepusha miradi hiyo kukosa tija kwa wananchi.

Mohamed aliwataka viongozi hao kutembelea mara kwa mara miradi hiyo ili kujiridhisha kama inatekelezwa kama ambavyo mikataba inaelekeza pamoja na kutoa maelekezo kwa wakandarasi.

"Hatutamvumilia mtu yeyote ambaye atakwamisha miradi ya maendeleo. Kwa hiyo nawaagiza wakuu wa mikoa yote nchini kusimamia utekelezaji wa miradi kwenye maeneo yao na kuchukua hatua za kisheria kwa wale watakaoonekana kukwamisha," alisema Mohamed.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo ya barabara, madaraja, vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya na miradi ya maji.

Pia aliwaagiza wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kufanya mikutano ya hadhara katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuelezea miradi ambayo serikali imetekeleza katika maeneo yao.

Alisema miradi inayotekelezwa na serikali kwenye maeneo ya wananchi ndiyo itakayokisaidia chama hicho kuaminiwa na wananchi na kushinda kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Mjumbe wa NEC Taifa anayewakilisha mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alisema kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo uliofanyika mkoani Mbeya, CCM kitaendelea kushinda kwenye chaguzi.

Alisema yeye kwa kushirikiana na viongozi wengine wa chama hicho ngazi ya mkoa watahakikisha wanawaeleza wananchi mambo mazuri ambayo chama hicho kimeyafanya ili waendelee kukiamini.

Alisema mpaka sasa chama hicho katika mkoa huo wa Mbeya kipo salama kutokana na kuendelea kushikilia majimbo yote ya mkoa huo pamoja na kata mbalimbali.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Radio na Televisheni cha EATV, Regina Mengi (kulia), akimkabidhi Meneja Mwandamizi wa Bidhaa za NMB, Beatrice Mwambije, cheti cha shukrani wakati wa kongamano la EATV Kinara ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. Benki ya NMB ni miongoni mwa makampuni yaliyodhamini kongamano hilo. Kushoto ni wafanyakazi wa NMB. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Majaliwa awawashia moto ma-DC goigoi

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI Mkuu Kasimu Majaliwa, amewaonya wakuu wa wilaya kuhusu tabia ya kulala na kuwa wavivu badala yake amewataka kutimiza majukumu yao kwa kutatua kero za wananchi.

Majaliwa alitoa onyo hilo jana jijini Dodoma wakati akifunga mafunzo ya uongozi kwa wakuu wa wilaya 138 yaliyofanyika kwa siku sita ya kuanzia Machi 13, mwaka huu.

Alisema wakuu wa wilaya ni kiungo muhimu katika kuiletea nchi mafanikio hivyo wanapaswa kuwa jirani na wananchi na kutatua kero zao bila kusubiri serikali kuu. Alisema nchi haiwezi kufikia maendeleo ya kweli kama wakuu wa wilaya hawatatimiza majukumu yao ipasavyo kwa kuwa wako karibu zaidi na wananchi.

Kwa mujibu wa Majaliwa, wakuu wa wilaya wanapaswa kujua kila kitu kinachoendelea kwenye maeneo yao ya utawala, kufuatilia miradi iliyoko badala ya kukaa ofisini.

"Tunataka kujenga madarasa, bila mkuu wa wilaya hatuyapati kwa haraka, tunataka kuweka maji kwenye kijiji, bila mkuu wa wilaya hakuna kitakachowezekana. Jukumu lenu kubwa ni kuhakikisha ndoto ya Rais Samia (Suluhu Hassan) inatimia. "Mawaziri watapita kwenye maeneo yenu na wakuu wa wilaya mnatakiwa mtoe taarifa sahihi kulingana na miradi mnayoisimamia ili tujue nini kinaendelea. Lengo tunataka kuona, utendaji wako unaenda vizuri," alisema.

Waziri Mkuu alisema matarajio ya Rais ni kuona wanawahudumia wananchi na viongozi wa serikali walioko ndani ya wilaya na kuonyesha kutoridhika pale fedha inapokuwa imetumika kinyume cha matarajio pamoja na kufuatilia mienendo ya wananchi kwenye eneo yao.

"Lakini pia muwezeshe kupatikana kwa maendeleo kwenye wilaya zenu. Tunahitaji mabadiliko, umeingia juzi tunataka kuona mabadiliko, usiingie tu ofsini unakaa na kuandaa safari zisizo na umuhimu wowote.

"Pia hakikisheni mnahamasisha shughuli zote za maendeleo kwenye miradi ya elimu, afya, kilimo na miundombinu ya barabara. Hilo ni jukumu la mkuu wa wilaya," aliwakumbusha.

Majaliwa aliwataka wakuu hao wa wilaya kufahamu taarifa za fedha zinazoingia kwa wakurugenzi wa halmashauri kwa ajili ya miradi ya maendeleo na miradi inayotekelezwa ili iwe rahisi kufuatilia na kubaini kama kuna ubadhirifu wa fedha za serikali umefanyika.

Pia aliwataka wajenge utaratibu wa kutoa miongozo ya namna ya kufikia mafanikio kwenye maeneo yao ya kazi, kwani ipo inayotoka serikalini na wizarani.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, wakuu wa wilaya wanatakiwa kusimamia amani na usalama kwa kuwa wao ndio wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama kwenye wilaya wanazotoka.

"Rais anataka muunganishe serikali na wadau. Kuna sekta binafsi huko tunataka kuona zina uhusiano mzuri na serikali, viongozi wa dini pamoja na majirani wa ndani, hata nje ya nchi.

"Kwa mfano Kigoma, mkuu wa wilaya anatakiwa kuwa na uhusiano mzuri na mkuu wa wilaya kutoka nchi jirani pamoja na kuweka vikao vya ujirani mwema. Kwa wale walioko mipakani hapa nikiwauliza kwa nini hamfanyi vikao hivyo, hakuna majibu," alisema.

Kutofanya hivyo, alisema hawatalinda utamaduni wa nchi na kutaka wakaimarishe uhusiano pamoja na kushughulikia migogoro ya ardhi kati ya kijiji na kijiji. "Mkasimamie vyanzo vya mapato kwani tunahitaji kuwa na mapato mengi yanayotoka huko kwenu kwa kuwa ninyi ndio viongozi wakuu kwenye wilaya. Ingekuwa nchi tungesema Rais wa Wilaya. Lazima mfuatilie na mjiridhishe kiasi kinachopatika pamoja na fedha ya serikali inavyotumika.

"Simamieni utendaji wa kazi kwenye halmashauri. Tunajua zipo zenye migogoro mikubwa, kuna tatizo unakuta mkurugenzi wako amenuniwa, nyie ndio wasimamizi wa eneo hilo kafuatilieni," aliagiza.

Alisema Mkuu wa wilaya anatakiwa kujua madiwani wanachojadili kwenye vikao vyao pamoja na, kuingilia kati kwa maslahi ya taifa, na kusimamia utoaji wa huduma za jamii.

Aliongeza kuwa wanatakiwa kuhakikisha wanafunzi kwenye eneo lao wanakwenda shuleni, kutatua kero ya upungufu wa madarasa na kuyaongeza kulingana na makusanyo ya fedha zinazopatikana.

"Kwenye afya, huduma zinazotolewa ndivyo sivyo, mara nyingine madaktari wanaingia saa nne ofisini, wakati mkuu wa wilaya upo, hilo hapana.

"Hospitali za wilaya zina migogoro mingi. Unakuta watumishi wanagombana kila siku. Simamieni utoaji wa huduma za afya, wananchi wanalalamika dawa hazipo, uliza mmepata shilingi ngapi na katika kipindi gani? Na nyie mnajua serikali kila baada ya miezi mitatu inaleta fedha kwa ajili ya kununua dawa," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki alisema mafunzo hayo yamehusisha washiriki 139, kati yao, 37 ni wapya na wengine 102 ni wale wanaoendelea na nyadhifa zao.

"Baada ya kupata mafunzo haya, tunatarajia mkirudi kwenye vituo vyenu vya kazi, mtatekeleza yale yote mliyoyapata kwa kushirikiana na wengine ili kuharakisha utekelezaji wa shughuli za Serikai," aliagiza.

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa na Taasisi ya Uongozi, yalihusisha mada 17 zilizogusa masuala mbalimbali ambapo baadhi ya Mawaziri walishiriki kutoa mada.


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 21 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late: RAPHAEL MELEKIZEDEK MNDOLWA**

**By 1. AUGUSTINO RAPHAEL MNDOLWA**
**2. ......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 29TH day of MARCH..2023

Dated at Morogoro this 14TH day of MARCH..2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LOMAYANI LOSHILAA MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 841 DDF – TOYOTA IST.** Chassis No. **NCP600090591.** ENGINE No. **2N22687350.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/65463/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**MOHAMMED ENTERPRISES T LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 185 DHJ – BAJAJI BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/99303/2023.**

HABARI KITAIFA

## Tanzania yaisaidia Malawi kukabili kimbunga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TANZANIA imetoa msaada wa vitu mbalimbali vikiwamo vyakula na matibabu kwa ajili ya kuisaidia Malawi kukumbwa na janga la dhoruba ya kimbunga Freddy.

Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Luteni Kanali Gaudenitius Ilonda, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari.

"Kama mtakumbuka vizuri Machi 13, mwaka huu, kimbunga kiitwacho 'Tropic Freddy' kilichoambatana na mvua kubwa na upepo mkali, kiliikumba nchi ya Malawi, kiasi cha kutisha, maji yalitiririka katika vitongoji na kusomba nyumba na kuleta maafa.

Kimbunga hicho kimesababisha maafa makubwa kiasi cha kutangazwa kuwa ni janga nchini humo baada ya kusababisha vifo, kuharibu miundombinu, nyumba, mazao na athari zingine," alisema.

Kutokana na athari hizo, Kanali Ilonda alisema serikali ya Tanzania kwa kutambua ujirani mwema, ushirikiano na undugu na Malawi, imetoa misaada mbalimbali ya kibinadamu ili kusaidia nchi hiyo kukabiliana na janga hilo. Alisema JWTZ imepewa jukumu kushiriki bega kwa bega kupeleka msaada huo.

Kanali Ilonda alisema kutokana na jukumu hilo, Mkuu wa Majeshi, Jenerali Jacob Mkunda, ametoa maelekezo yanayoratibiwa na Mnadhimu Mkuu wa JWTZ, Luteni Jenerali Salum Othman na kwamba magari 37 ya jeshi hilo yataondoka Dodoma muda wowote kupeleka misaada hiyo Malawi.

"Baadhi ya magari hayo yanayopelekwa Malawi ni pamoja na gari la wagonjwa, karakana ya magari inayotembea na malori makubwa 10 yenye uzito wa tani 18," alisema.

Pia alisema magari hayo yatasafirisha msaada wa mahema, mablanketi, chakula na mahitaji mengine ya kibinadamu yanayotolewa na serikali Tanzania.

Alisema sambamba na hilo, JWTZ inapeleka helkopta mbili ikiwa ni sehemu ya msaada unaotolewa na serikali kusaidia katika janga hilo.

"Hivi punde helkopta hizo zimeruka kutoka Dar es saalam kuelekea Malawi tayari kuanza utekelezaji wa majukumu hayo," alisema.

# Zitto awakaba koo polisi watu kupotea

**Na Julieth Mkireri,** KIGOMA

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, ametoa saa 24 kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma na Ofisa Usalama wa Mkoa, kueleza wapi walipo vijana watatu wanaodaiwa kupotea.

Wakati Zitto akiagiza hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Philemon Makungu, alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu kuhusiana na hilo, alisema: "Kama ameongea kwenye mikutano hayo sasa si ya kwenye mikutano? Sisi tunaendelea na mambo yetu kama kawaida. Kama kutuandikia si angetuandikia?"

Akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Kigoma mjini, Zitto alisema amepata taarifa za upotevu wa vijana hao ambao hawajulikani waliko hadi sasa.

Zitto alisema viongozi hao wenye dhamana wanatakiwa kutoa taarifa za watu hao walipo kinyume cha hapo, chama chake kitachukua hatua zaidi ili haki ipatikane.

"RPC na ofisa usalama wasije na mambo ya kuteka watu, yamepitwa na wakati. Tunataka waseme watu wetu wamekwenda wapi? Hatutaki haya mambo yarudiwe na haya mambo yameshapitwa na wakati," alisema.

Kiongozi huyo alisema chama hicho kinataka nchi iendeshwe kwa misingi ya sheria na kama kuna mtu amefanya makosa, akamatwe kwa taratibu za kisheria na si kuteka.

"Hatutaki tena tuanze kudai uchunguzi kama tunavyodai Kibiti na Mkuranga. Tafadhali RPC na Ofisa Usalama tupate taarifa hawa watu wako wapi Ndani ya masaa 24, vinginevyo hatua tutakazochukua tusilaumiane," alisisitiza.

Akiwa mjini Kasulu, Zitto alimwagiza Waziri Kivuli wa Kilimo na Mifugo wa chama hicho, kufuatilia ardhi iliyochukuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na kuuzwa kwa baadhi ya matajiri.

Zitto alisema ardhi hiyo ilirudishwa kwa wananchi na sio kwa ajili ya halmashauri kuanza kuigawa na kuiuza kwa watu matajiri.

"Ardhi ile haikutolewa ili iwe chanzo cha mapato cha halmashauri ilitolewa kwa ajili ya wananchi ambao muda wote wanahitaji kufanyia shuguli za kilimo.

"Hatuwezi kuendelea kuwa manamba, Wajerumani walitufanya manamba, Waingereza vivyo hivyo na sasa tena kurudi kwenye zama za awali, jambo hilo haiwezekani, hatuwezi kukubali katika hili," alisema.

Zitto alisema Rais alitoa eneo hilo kwa ajili ya wananchi na kwamba wataipambania irudi kwa walengwa ili wafanye shughuli zao za maendeleo.

"Wakati eneo lile linatolewa hapakuwa na nyaraka yoyote kwa serikali kwamba, ardhi hiyo wapewe halmashauri, ardhi ile ni kwa ajili ya wananchi na ni lazima irudi kwao," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Zitto, jambo hilo ni lazima watalifuatilia na kwamba watafika Kasulu ili wapate idadi ya wananchi wawapiganie wapate ardhi yao na sio wao kugeuka kuwa vibarua kwenye mashamba ya matajiri.

"Haya mambo ya kuendesha serikali kibabe ni lazima tuyakomeshe, mimi sijali vyama, ninaaangalia maslahi ya wananchi, mapambano ya kisiasa ni muhimu kulinda haki zenu, tuimarishe chama na kujipanga kwa chaguzi zijazo," alidai.

Aliwasihi wakazi wa Kasulu kushirikiana kuimarisha chama badala ya kujikita kumpenda mtu ambaye anaweza akaondoka na chama kikaendelea kuwapo.

Mgombea wa urais kupitia chama kikuu cha upinzani cha CNL cha Burundi, Agathon Rwassa, alimpongeza Rais Samia Suluhu kwa kuridhia kufanyika kwa mikutano ya vyama vya siasa na kukipongeza ACT Wazalendo kwa kaulimbiu yake ya 'Taifa la Wote Maslahi kwa Wote.'



Mhandisi wa Vikosi vya Ujenzi, anayejenga jengo la Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Mwesigwa Ichwekeleza (kulia), akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge Elimu na Michezo, ilipotembelea kuona maendeleo ya Chuo hicho Kigamboni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri ataka rejista migogoro ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula amewataka wakuu wa wilaya nchini kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na rejista ya migogoro ya ardhi ili kujua chanzo na mikakati ya utatuzi wa migogoro hiyo kila inapojitokeza.

Waziri Mabula alisema hayo jana wakati wa uwasilishaji wa mada yake kwa wakuu wa Wilaya wanaoshiriki mafunzo yanayoendelea Jijini Dodoma chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. "Natambua kuwa kila mkuu wa wilaya anapoteuliwa migogoro ambayo ilishapatiwa ufumbuzi huwa inaanza upya ndiyo maana nawataka kusimamia uanzishwaji wa rejista za migogoro ya ardhi itakayosimamiwa na wakurugenzi ili kudhibiti na kumaliza,' alisema.

Katika mada yake, Dk. Mabula alisema kumekuwapo na changamoto kwenye halmashauri ya kutodhibitiwa kwa migogoro ya ardhi na kutosimamia mipango ya matumizi ardhi iliyoandaliwa mijini na vijijini.

Changamoto nyingine, alisema ni halmashauri kutoshiriki kikamilifu kwenye mikakati ya makusanyo yanayotokana na sekta ya ardhi pamoja na bajeti ndogo ya kutekeleza majukumu ya sekta na kutokutengwa kwa ardhi ya uwekezaji.

Pia aliwataka viongozi hao wa wilaya kusaidia katika kuongeza hamasa kwenye suala la ukusanyaji wa mapato ya serikali yanayotokana na sekta ya ardhi ikiwamo kusimamia mikakati ya ukusanyaji maduhuli na kuwakumbusha wananchi kutumia fursa iliyotolewa na Rais ya msamaha wa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi inayoishia Aprili 30, mwaka huu. Sambamba na hiyo, Dk. Mabula amewataka viongozi hao kusimamia Halmashauri ili zitenge fedha kwenye bajeti kuhakikisha ardhi inapangwa, kupimwa na kumilikishwa huku akiwahimiza kutambua kuwa mamlaka za upangaji ardhi ziko chini ya halmashauri.

'Halmashauri zitambue kuwa jukumu hilo bado ni lao na wanahitaji kuendelea kushiriki kikamilifu kwenye kutenga fedha ili kutekeleza majukumu yao na kuwawezesha watumishi waliopo katika Halmashauri kufanya kazi kwa mujibu wa taaluma zao," alisema.

Waziri Mabula pia alidokeza kuwa kuna baadhi ya halmasahauri nchini ambazo zimetumia mikopo ya Sh. milioni 50 iliyotolewa na Rais kwa baadhi ya halmashauri ili zitumike kupima, kupanga na kumilikisha ardhi lakini baadhi zilielekeza fedha hizo katika matumizi mengine bila kuzingatia kusudio la mikopo hiyo.

Kwa muktadha huo, aliwaelekeza wakuu wa wilaya kusimamia eneo hili ili wakurugenzi wa halmashauri watumie mikopo hiyo kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na hatimaye kurejesha fedha hizo ili halmashauri zingine zikopeshwe.

# Kampuni Congo kutangaza the Royal Tour

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, ameipongeza na kuishukuru kampuni ya mabasi ya Classic Coach kwa uamuzi wake wa kutangaza filamu ya The Royal Tour.

Filamu hiyo iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kifaransa, itaonyeshwa katika mabasi ya kampuni hiyo yanayosafirisha abiria katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kiongozi huyo alitoa pongezi hizo, kwenye hafla ya uzinduzi wa uonyeshaji wa filamu hiyo kwenye mabasi hayo iliyofanyika kwenye viwanja vya ubalozi wa Tanzania nchini DRC, Kinshasa jana na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo maofisa wa Ubalozi wa Tanzania na wawakilishi wa kampuni hiyo.

Pia alimpongeza Balozi wa Tanzania DRC, Said Mshana, na timu yake kwa kufanikisha jambo hilo alilosema ni la muhimu na la kuungwa mkono.

Dk. Tax alisema balozi huyo ana mwaka mmoja tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo lakini katika kipindi hicho kifupi amefanikisha mambo mengi makubwa na muhimu.

"Amefanya mambo makubwa likiwamo hili la kuishawishi kampuni ya Classic yenye mabasi 50 inayotoa huduma ya usafiri wa abiria katika miji mbalimbali ya Congo, ikiwamo ya Kinshasa na Lubumbashi, kutangaza filamu ya the Royal Tour bila malipo," alisema.

Alisema mabasi ya kampuni hiyo inayomilikiwa na Mtanzania Amir Abdallah, anayeishi nchini humo hayatumiwi na Wacongo pekee, bali na raia wa nchi zingine, hivyo ni fursa katika kutangaza Tanzania na uwekezaji, biashara pamoja na utalii ili kutimiza azma ya serikali ya kuvutia watalii milioni tano na mapato ya Dola za Kimarekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025.

Pia alitoa wito kwa kampuni zingine na sekta binafsi kwa ujumla kujitokeza kushirikiana na Serikali katika jitihada za kukuza uchumi ikiwa ni pamoja na kuchangamkia fursa za uwekezaji zinazopatikana Tanzania.

Waziri huyo kwenye hotuba yake, alisema hafla hiyo ni sehemu ya kusherehekea miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Tanzania Machi 19, 2021 na mafanikio mengi yamepatikana katika kipindi hicho cha uongozi wake.



Ofisa Mkuu Masoko wa Kituo cha Uwekezaji, UTT AMIS, Martha Mashiku (kulia), akigawa vinywaji kwa wanafunzi wa Shule ya Mtoni Maalum, inayofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili na Usonji wakati wa kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe aongoza mamia kumuaga mwasisi CHADEMA

**Na Vitus Audax** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ameongoza mamia ya wanachama wa chama hicho na waumini wa Kanisa Katoliki katika ibada ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini na mwasisi wa chama hicho, Syilvester Masinde.

Ibada hiyo ilifanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Watakatifu Petro na Paulo Mwananchi iliyoko Kata ya Mahina wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na Katibu Mkuu John Mnyika, John Heche, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Maulida Komu, na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mohammed Ali Mohammed aliyemuwakilisha Mwenyekiti wa Taifa, Samia Suluhu Hassan.

Ibada hiyo iliongozwa na mapadri Christian Nuhu, Denis Mihayo, Mpere Rambe na Paroko wa Parokia hiyo, Padri Kayembo Lusenge.

Akizungumza katika ibada hiyo, Mbowe alisema chama hicho kimepoteza mtu muhimu na mwalimu wa muda wote wa viongozi na wanachama.

Pia alisema CHADEMA imepoteza maktaba yenye uwezo mkubwa wa akili katika kuandaa na kuandika vitabu na makala mbalimbali kudai haki, amani na maendeleo kwa manufaa ya chama na taifa kwa ujumla.

"Chama chetu tunaamini katika familia ya CHADEMA isiyo na mipaka katika nyanja yoyote ya kichama, kidini wala kiitikadi kwa namna yoyote ile na imani hiyo ndiyo aliyosimama nayo mzee wetu na mlezi wetu Masinde," alisema Mbowe

Pia alisema Masinde alikilea chama hicho pamoja na viongozi wake kwa wakati wote akiwa hai pamoja na yeye mwenyewe alimlea kichama tangu akiwa mdogo wakati wa kuanzishwa kwa chama hicho.

"Mzee Masinde aliamini katika maneno manne ambayo ni uhuru wa watu, demokrasia, haki za wananchi na maendeleo ya wananchi wote," alisema. Katika hatua nyingine, Mbowe, alitoa pongezi zake kwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ruhusa kwa Mwenyekiti wa UVCCM, Mohamed Ali Mohamed, kushiriki katika ibada hiyo ya kumuaga mpendwa wao.

Alisema suala la kuungana na wanachama wa chama hicho katika kipindi hiki kigumu ni faraja kwa wanachama wa CHADEMA pamoja na wanafamilia kwa ujumla.

Mohamed, akiwasilisha salamu za rambirambi kutoka kwa Rais Samia alisema chama hicho kitakuwa pamoja na wanafamilia na wanachama wa CHADEMA katika kipindi cha majonzi kwa kuwafariji bila kujali tofauti zao za kiitikadi.

Akiendesha ibada hiyo, Padri Lusenge aliwataka wanafamilia, ndugu na jamaa kubaki katika imani wakati wote na kumwombea Masinde wakati wote ili apumzike mahali pema.

Alisema kila nafsi itaonja mauti, hivyo kila mmoja anatakiwa kuishi katika imani na kutenda mema ili siku yake ikifika apumzishwe katika sehemu inayostahili.

Masinde alifariki dunia Machi 15, mwaka huu, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando alipokuwa akipatiwa matibabu ya tezi dume.

# Bil. 648/- zakusanywa mapato ya halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amesema Sh. Bilioni 648.12 sawa na asilimia 91 ya malengo zimekusanywa kama mapato ya ndani katika ngazi ya halmashauri.

Kairuki aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa baraza la wafanyakazi wa ofisi hiyo uliofanyika jijini hapa.

Alisema kiasi hicho ni kati ya makadirio ya Sh. bilioni 714.48 zilizotarajiwa kukusanywa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Februari, mwaka huu.

Kairuki alisema mapato hayo ni kutoka vyanzo mbalimbali kama ushuru wa mazao, huduma, magulio, masoko, ada za uchangiaji huduma za afya na vyanzo vingine.

Alisema kwa kipindi hicho kumekuwa na mafanikio mbalimbali ambayo yamepatikana kwenye ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mabaraza kwa shule za msingi na sekondari, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kutokana na sera ya elimu bila ada na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba, kidato cha nne na cha sita.

Kairuki aliagiza mikutano ya baraza la wafanyakazi wa ofisi hiyo itumike kujadili malengo na mipango ya taasisi na maslahi ya watumishi na kuwakumbusha hakuna haki bila wajibu hivyo kuwataka watendaji hao kuhakikisha utendaji kazi wao unakuwa wa tija, weledi na uwajibikaji ili kuiwezesha serikali kuongeza mapato hivyo kuwezesha utoaji wa maslahi bora.

"Mikutano ya baraza iwe na kazi ya kujadili utendaji kazi wa kila siku na jinsi ya kuboresha utendaji kazi zaidi, tija na maslahi lazima viwe na uwiano ili kuwa na matokeo bora ya utendaji kazi unaolenga kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi," alisema.

Pia alisema ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha vifo na kuligharimu taifa kwa kupoteza nguvu kazi muhimu aliwahimiza watendaji hao kuchukua tahadhari kwa kufanya mazoezi na kuzingatia lishe bora.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Adolf Ndunguru, alisema baraza hilo litajadili mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23, na mapendekezo ya mpango wa bajeti ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2023/24.

HABARI KITAIFA

# Vishoka kikwazo taaluma uuguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSAJILI wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), Agnes Mtawa, amesema vitendo vya uvunjifu wa maadili kwa wauguzi na wakunga vishoka ambao wamekuwa wakijiingiza katika taaluma hiyo bado ni kikwazo katika sekta ya afya nchini.

Mtawa alisema hayo jana jijini hapa wakati wa mahafali ya saba na utoaji wa vyeti vya usajili na leseni kwa wauguzi na wakunga zaidi ya 1,000 waliofanya vizuri kwenye mitihani iliyoandaliwa na baraza hilo.

"Pamoja na mafaniko tuliyoyapata bado ziko changamoto mbalimbali vikiwamo vitendo vya uvunjifu wa maadili kwa wauguzi na wakunga. Lakini pia liko tatizo la watu ambao si wanataaluma kuingilia taaluma yetu," alisema.

Pia alisema wauguzi na wakunga wanapaswa kuzingatia maadili ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mbalimbali ili kuisaidia serikali kupunguza vifo vya mama na mtoto.

"Sisi tutaendelea kuchukua hatua kwa muuguzi au mkunga yeyote ambaye atabainika kuwa amekiuka maadili kwa kumfuta kwenye usajili wetu," alisema.

Sambamba na hilo, alisema tangu mwaka 2016 wauguzi na wakunga 50 walibainika kuvunja maadili ya utumishi wa umma ambapo kati yao wanne walifutiwa usajili wao na kupokonywa leseni na wengine kupewa karipio kali.

Pia alisema pamoja na kero hiyo ya ukiukaji wa maadili ya kada hiyo bado kuna kero ya wauguzi na wakunga vishoka ambao si wanataaluma.

"Bado wako wananchi ambao wanajifanya wanataaluma hii na kutoa huduma bila ya kuwa na vigezo hili ni kosa la jinai ambao tumekuwa tukiwabaini tumewachuklia hatua za kuwapeleka mahakamani na wengine tayari wameshafungwa vifungo mbalimbali," alisema Mtawa.

Kadhalika, alisema ili kukabilina na kero hiyo, baraza limeandaa mfumo ambao amewapatia waajiri ili waweze kuhakiki usajili wa wauguzi na wakunga.

"Mfumo huu una uwezo wa kubaini muuguzi au mkunga aliyesajiliwa na asiyesajiliwa, hivyo nitoe wito kwa waajiri kufanya uhakiki kupitia mfumo huu mara kwa mara ili kukabili changamoto ya watu wasio wanataaluma kujipenyeza," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
BODI YA MFUKO WA BARABARA



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

SALAMU ZA PONGEZI

**Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara** wanaungana na Watanzania wote kukupongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wako.

**Ndani ya Kipindi cha Miaka Miwili:**

- Umeongeza bajeti ya kugharamia matengenezo ya barabara kwa asilimia 27 kutoka Shilingi bilioni 806.7 mwaka wa fedha 2019/20 hadi Shilingi bilioni 1,027 mwaka wa fedha 2021/22.
- Umewezesha zaidi ya kilometa 50,000 za barabara za Kitaifa na Wilaya pamoja na madaraja kufanyiwa matengenezo kila mwaka.
- Umewezesha sehemu kubwa ya mtandao wa barabara kupitika wakati wote. Asilimia 90 na asilimia 60 ya barabara za Kitaifa na Wilaya, mtawalia, ziko kwenye hali nzuri na wastani.
- Umefungua barabara nyingi za vijijini kwa kutenga zaidi ya Shilingi bilioni 440 kila mwaka kugharamia maboresho ya barabara za Wilaya.
- Umewezesha zaidi ya wanawake 4,000 kupata ajira za muda kwenye kazi za matengenezo ya barabara za Wilaya.

*Kazi Iendelee*

*Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara tunakutakia kila lakheri kwenye Uongozi wako mahiri na uliotukuka*

Bodi ya Mfuko wa Barabara, Makao Makuu Dodoma, 11 Barabara ya AMMAR, 41107 DODOMA MAKULU, DODOMA
Simu : +255 26 2963277-8, Nukushi: +255 26 2963279-80, Barua pepe: info@roadsfund.go.tz, Twitter: @rfb_tz, Facebook: www.facebook.com/RFBTZ/, Instagram: @rfb_tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rais Samia ameonyesha uwezo mkubwa kiuongozi, aungwe mkono

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, leo anatimiza miaka miwili tangu aliposhika dhamana ya kuiongoza Tanzania baada ya aliyekuwa anashika nafasi hiyo, Dk. John Pombe Magufuli, kufariki dunia.

Pamoja na kushika nafasi hiyo, Rais Dk. Samia pia ameandika rekodi ya aina yake ya kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kushika madaraka hayo ya juu ya uongozi wa nchi na kuwathibitishia Watanzania na dunia nzima kuwa wanawake wana uwezo mkubwa kama walivyo wanaume au zaidi, pindi wanapopewa nafasi ya uongozi.

Ni ukweli usiofichika kuwa Rais Samia katika miaka miwili ya uongozi wake, amefanya mambo makubwa ambayo yamesababisha kupata nishani ya uongozi bora nchini Afrika Kusini alipokuwa katika ziara ya kikazi hivi karibuni. Sambamba na nishani hiyo, alitunukiwa shahada ya udaktari wa heshima (Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ikiwa ni kutambua mchango wake katika uongozi na maendeleo ya nchi.

Yako mambo mengi ambayo ameyafanya ikiwamo kuendeleza yale yaliyoanzishwa na mtangulizi wake kama vile miradi ya kimkakati ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na mradi wa umeme wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere katika Mto Rufiji.

Miradi mingine ni ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji kama vile barabara, viwanja vya ndege, bandari pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya na mikoa pamoja na miradi ya maji katika maeneo mbalimbali. Mbali na miradi hiyo, Rais Samia katika uongozi wake pia ameongeza bajeti kama sekta mbalimbali zikiwamo afya, kilimo, miundombinu, elimu na maji.

Jambo lingine ambalo ni la kupigiwa mfano ni kuitangaza Tanzania kimataifa hususan vivutio vya utalii kupitia filamu ya The Royal Tour ambayo ameicheza mwenyewe ikiwa ni jitihada za kukuza sekta ya utalii kwa kuwavutia watalii kutembelea vivutio hivyo na kuwekeza kwenye miundombinu ya hoteli.

Licha ya filamu hiyo, Rais Samia amefungua milango katika medani ya uhusiano wa kimataifa kwa kurejesha uhusiano wa kikanda na kimataifa uliokuwa umedorora. Kwa kufanya hivyo, ameifanya Tanzania kurejea katika anga za kimataifa hususani katika masuala ya kidiplomasia.

Jambo kubwa na la msingi, ni hatua yake ya kufungua milango kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara ambayo ilipigwa marufuku kwa takriban miaka saba, huku akisisitiza Watanzania kufanya siasa za kistaarabu na kudumisha umoja, amani na mshikamano. Kimsingi amesisitiza kuwa vyama vya siasa au tofauti yoyote ya rangi au imani visiwe chanzo cha Watanzania kubaguana au kuchukiana.

Hivi sasa, vyama vya siasa vinafanya mikutano katika maeneo mbalimbali huku vikiibua mambo mbalimbali ambayo kwa kiasi kikubwa yanakisaidia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali yake kuchukua hatua ili kurekebisha kasoro mbalimbali zinazojitokeza.


Kwa ujumla, Rais Samia amefanya mambo makubwa ndani ya kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake. Ni vyema wateule wake katika ngazi mbalimbali wanaomsaidia kuleta maendeleo ya wananchi kufanya yale ambayo amedhamiria ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Zaidi ya hayo, Dk. Samia ameonyesha kuwa wanawake wana uwezo mkubwa katika kuleta mabadiliko na maendeleo katika jamii. Kwa mantiki hiyo, ni wakati sasa kwa wanawake kuonyesha kwa vitendo kuwa wanaweza kufanya mambo makubwa ndani ya jamii. Kwa wale waliopewa nafasi katika ngazi mbalimbali, wanapaswa kuonyesha kwa vitendo ili waendelee kuaminiwa zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka miwili ya Samia, vyama vya upinzani vimetabasamu

**KATIKA** kipindi cha miaka saba, vyama vya upinzani vilikuwa kwenye sintofahamu, baada ya kuwapo kwa zuio la mikutano ya hadhara ambalo lilisababisha viongozi wa vyama hivyo wasikutane na wanachama wao.

Lakini kwa miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa madarakani, ambayo inatimia leo, amefanikiwa kuondoa zuio hilo, na kuvifanya kuwa huru kuendelea na mikutano hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

Ruhusa hiyo ilitolewa Januari 3 mwaka huu, tarehe ambayo ninadhani inaweza kuwa ya kukumbukwa na viongozi wa vyama hivyo, kwani ndio ambayo Rais alitangaza kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Tarehe hiyo Rais alikutana na viongozi wa vyama vya siasa, huku akiridhia mambo kadhaa, katika medani za siasa nchini, ambayo yalikuwa kilio kikubwa na cha muda mrefu kwa viongozi wa vyama vya upinzani.

Katika mkutano huo, Rais aliruhusu rasmi mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, lakini akisisitiza zaidi siasa za kistaarabu na kuepuka kejeli na matusi, huku akibainisha kuwa tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara limeondoshwa.

Ruhusa ya mikutano ya hadhara, imeonekana kuwa neema kwa vyama vya upinzani, hasa vya CHADEMA na ACT-Wazalendo, ambapo viongozi wake kwa sasa wanaendelea na mikutano katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mikutano hiyo inakwenda sambamba na kupata wanachama wapya wanaotoka katika vyama vingine na wale ambao hawajawahi kuwa na vyama, hali inayoonyesha kuwa miaka miwili ya Rais vyama hivyo vimefaidi.

Vyama vya upinzani vimefaidi, kutokana na ukweli kwamba, muda wa miaka saba ambayo vilikuwa vifungoni, havikuweza kupata nafasi ya kutangaza sera na kuingiza wanachama wapya kama inavyofanyika sasa.

Awali haikuwa rahisi viongozi wa vyama hivyo kukutana na wanachama wao au kupata nafasi ya kutoa elimu ya uraia kwa wananchi, lakini sasa vimepata nafasi hiyo na siyo kuishia katika vikao vya ndani.

Lakini katika hali isiyotarajiwa, Rais Samia ameondoa zuio na kuruhusu vyama kuendelea na shughuli kama kawaida, kwa kuwa anaamini nchi inajengwa na wote bila kujali itikadi za vyama wanavyotoka, dini au kabila.

Mkazo wa Rais ni kutaka kufanya taifa liwe kitu kimoja na kuwapo na maridhiano yanayoendana na ustahimilivu, mabadiliko na kujenga upya nchi, kwa manufaa ya Watanzania wote.

Ni wazi vyama vya upinzani vitakuwa vinamshukuru Rais hata kimoyomoyo kwa uamuzi huo wa kuvitoa, katika kifungo ambacho kilisababisha vibaki vinanung'unika kimya kimya baada ya kushindwa kufurukuta.

Mwenyekiti wa Taifa wa (CHADEMA), Freeman Mbowe, yeye hajasita kumsifia Rais hadharani kwa uamuzi huo wa kuondoa zuio la mikutano, na kwamba hatua hiyo itasaidia kuchochea uchumi wa taifa.

Mbowe alisema hayo Januari 21, 2023 wakati akizungumza kweye mkutano wa kwanza wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Furahisha uliopo Wilaya ya Ilemela Jijini Mwanza.

Alisema: "Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni" huku akikiri kuwa Rais ni msikivu, anatambua umuhimu wa kuwa na demokrasia nchini na kutaka Watanzania waendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumuongoza ili azidi kuongoza taifa katika misingi mizuri.

Ukweli ni kwamba, inabidi viongozi wa vyama vya upinzani washukuru, kwani miaka saba bila mikutano ya hadhara inawezekana ulikuwa ni mtihani mgumu ambao huenda ulisababisha washindwe kusajili wanachama wapya.

## SAFU

### FIKRA MBADALA

# Kwa miaka hii miwili ya Rais Samia mabadiliko ya Katiba yanawezekana



**Pascal Mayalla**

JUMAPILI ya leo, Machi 19, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anatimiza miaka miwili tangu alipoingia madarakani. Ndiyo siku aliyokula kiapo cha kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na kifo cha aliyekuwa katika nafasi hiyo, Dk. John Pombe Magufuli.

Kwa ujumla, Machi ni mwenzi muhimu sana kwa historia ya taifa letu la Tanzania. Ni mwezi kihistoria wa kumbukumbu mbaya ambao kwa mara ya kwanza, taifa lilimpoteza kiongozi wetu Mkuu, Dk. Magufuli, maarufu kama JPM. Ni rais wa kwanza nchini kufariki dunia akiwa madarakani, hivyo ni mwezi kihistoria wa kumbukumbu mbaya na chungu ya kumpoteza shujaa wetu huyu. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Pamoja na hayo, mwezi huu pia ni mwezi wa historia, kumbukumbu nzuri na tamu kwa Tanzania kupata Rais wa kwanza Mwanamke, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye leo anatimiza miaka miwili madarakani. Kwa hiyo ni mwaka wa ukombozi wa mwanamke na kwa vile Rais Samia ameupata urais kwa kudra tu za Mwenyezi Mungu, akashauri uchaguzi wa 2025 Watanzania sasa twende tukachague Rais mwanamke.

Katika miaka hii miwili, Rais Samia amefanya mengi, makubwa na mazuri kwenye nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lengo la makala hii si kuzungumzia mafanikio ya Rais Samia na mambo makubwa aliyoyafanya bali kumsaidia na kumshauri kuwa kuna jambo kubwa muhimu kuliko jambo lolote kwa taifa lolote ambalo anapaswa kulifanya kabla ya kuhitimisha awamu yake ya kwanza mwaka 2025.

Kilio kikubwa cha kisiasa kwa sasa ni Katiba Mpya lakini kwa muda wa takriban miaka miwili uliobaki kwa Rais Samia kukamilisha awamu yake ya kwanza, hautoshi kwa mchakato wa kutupatia katiba mpya bora, vinginevyo tutake bora katiba. Hata hivyo, kwa muda huu uliobaki, unatosha kabisa kufanya mabadiliko ya katiba kwa ari ya 'linalowezekana leo, lisingoje kesho'.

Nizungumzie kidogo ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais anapewa ushauri kwa njia kuu mbili, ambazo ni ushauri rasmi na ushauri usio rasmi. Ushauri rasmi ni ule unaotolewa na washauri rasmi, Serikali, Bunge na Mahakama, wasaidizi wake, wakuu wa taasisi na vyombo vyake. Kawaida, ushauri huu huwa mara nyingi unakuwa kwa maandishi.

Ushauri usio rasmi ni mwingine wowote ambao Rais wetu anaweza kushauriwa na yeyote kwa njia yoyote, tukiwemo sisi waandishi wa habari na vyombo vya habari, wasanii, wanamuziki au wananchi wa kawaida. Enzi za JPM wananchi walitumia mabango, wasanii walitumia sanaa, wanamuziki walitumia nyimbo na sisi waandishi tulitumia kalamu zetu.

Kuna wengi wanadhani kwa vile Rais wa nchi ana washauri rasmi, basi hao ndio wanaomshauri vizuri au kwa usahihi bila kujua kuwa kuna uwezekano ushauri usio rasmi ukawa na manufaa kwa taifa letu kuliko hata ushauri rasmi. Mfano mzuri ni kwa vile nchi yetu inaongozwa na katiba, wasaidizi wa Rais walipaswa kuijua katiba na kumshauri ushauri stahiki.

Lakini kama washauri waliopaswa kuijua katiba, hawaijui katiba kikamilifu, ikitokea Rais wetu akakiuka katiba bila ya yeye kujua, na wanaopaswa kuijua katiba ili kumshauri Rais wetu, ama hawajui au wanajua lakini wanamwogopa kumwambia katiba hairuhusu jambo fulani, watu pekee wa kumshauri Rais ni sisi wananchi wa kawaida na hiki ndicho ninachokifanya hapa.

Katiba ndio sheria mama na sheria nyingine yoyote ikipingana na katiba basi inakwenda kinyume cha katiba na inakuwa sheria batili.

Mamlaka ya kuibatilisha hiyo sheria inayokinzana na katiba ni katiba yenyewe na si Mahakama Kuu. Kazi ya Mahakama Kuu ni kutamka tu kuwa sheria fulani ni kinyume cha katiba na baada ya tamko hilo, ubatili huo unakuwa tayari umeishabatilika. Kazi inabaki kwa serikali na bunge kuufuta ubatili huo kutoka kwenye vitabu vya sheria.

Nimesema wasaidizi na washauri wa Rais walipaswa kuijua katiba lakini hawaijui ndio maana baadhi ya wanasheria wetu na serikali yetu (si awamu hii ya Rais Samia), walitunga sheria fulani yenye kipengele batili, kinachokwenda kinyume cha katiba ya nchi, Bunge letu likaitunga sheria hiyo batili na Rais akaitia saini sheria hiyo batili ambayo inaendelea kutumika mpaka leo.

Mchungaji Christopher Mtikila (Mungu amweke mahali pema peponi) alifungua shauri kupinga kipengele hicho, akashinda, mahakama ikakitamka kipengele hicho ni batili.

Serikali ikakata rufani kupinga hukumu hiyo na wakati huo huo kufanya mabadiliko ya Katiba ya JMT ya mwaka 1977 na kukichomekea kipengele hicho ndani ya katiba yetu.

Kwenye ile rufani serikali ilishindwa na Mchungaji Mtikila akafungua shauri lingine kupiga mabadiliko hayo ya katiba, na akashinda tena kwa Mahakama Kuu kutangaza mabadiliko hayo ni batili kwa sababu yameingiza ubatili ndani ya katiba yetu.

Serikali ikakata rufani kupinga hukumu hiyo na Mahakama ya Rufani ikatamka kwa lugha ya Kiingereza "The Court is not the custodians of the will of the people", the will of the people ni katiba, kumaanisha Mhimili wa Mahakama si mlinzi wa katiba, hilo ni jukumu la Mhimili wa Bunge. Kwa hiyo suala hilo lilirudishwa Bungeni kitu ambacho si sahihi. Mpaka leo ubatili ule bado uko kwenye sheria zetu na ndani ya katiba yetu.

Kwa mambo makubwa mazuri Rais Samia anayoyafanya, naamini kabisa ndani ya moyo wake kwa kauli na matendo, amekubali mchakato wa katiba mpya kujadiliwa lakini kipindi cha miaka miwili kufikia uchaguzi wa 2025 ni kifupi kuipata, hivyo mchakato wa katiba mpya utawekwa kiporo na kuingizwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025 -2030.

Kwa vile ubatili kwenye katiba yetu ulichomekewa kiubatili kwa hati ya dharura, ikimpendeza Rais Samia anaweza kabisa kukiondoa kipengele hicho batili ndani ya katiba yetu kwa kutumia hati ya dharura kama walivyokichomekea, kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025. Hili linawezekana kabisa. Linalowezekana leo, lisingoje lesho.

Hongera Mama Samia kutimiza miaka miwili madarakani.

Mungu Mbariki Rais Samia
Mungu Ibariki Tanzania

**Paskali 0754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

## MIAKA MIWILI YA SAMIA:

# Tufungue bandeji madonda yamepona



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

LEO ni Jumapili ambayo Watanzania wana kila sababu ya kutathmini nini kimefanyika katika miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni Rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi hii, akipenda kujitambulisha kama Rais mwenye maumbile ya kike.

Utambulisho wake huo, unatokana na ukweli kuwa amethibitisha kumbe wanawake wanaweza kufanya kile ambacho baadhi ya wanaume hushindwa kukifanya.

Rais Samia aliingia madarakani Machi 19, 2021 kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ikiwa ni baada ya mtangulizi wake, Rais wa Tano, Dk John Magufuli, kutangulia mbele za haki.

Kuondoka kwa Dk. Magufuli duniani, ndiko kulikoiandikia Tanzania historia ya kuongozwa na mwanamke katika jamii hii ambayo hakika ililemea katika mfumo dume kwa miaka mingi tangu kupata uhuru mwaka 1961. Mfumo dume huo ndio ulisababishia baada ya Dk. Magufuli kufariki dunia, watu kuingiwa na wasiwasi wa nani atarithi mikoba yake licha ya Katiba ya nchi kutamka wazi wazi ni nani angechukua nafasi pindi litokeapo la kutokea.

Inasemekana watu waliojitia upofu, waliamini kwamba ungefanyika uchaguzi mwingine na kupatikana Rais mwanamume, hivyo Samia kuendelea kuwa Makamu wa Rais. Ulikuwa upofu wa kujipangia.

Sintofahamu hiyo, ndiyo iliyomfikisha hata Rais Samia kujitambulisha kuwa Rais katika maumbile ya kike, akiwathibitishia wahafidhina hao kuwa anaweza na kweli akaweza.

Katika miaka yake hii miwili madarakani ambayo kwa kweli ni mfupi, Rais Samia amefanya hata ambayo hayakutarajiwa na wengi na ameituliza nchi, tofauti na matarajio ya wengi kwamba asingeweza hasa kutokana na mazingira magumu alimopitia.

Ikumbukwe kuwa alichukua uongozi wa nchi katika kipindi kigumu cha janga la UVIKO-19 ukiwa ni wakati ambao mtangulizi wake alishapandikiza mbegu ya kutoamini uhalisia wa ugonjwa huo, hata kufikia wakati akidharau barakoa na chanjo.

Ni wakati huo ambao Dk. Magufuli alikataa kupokea chanjo akiamini kuwa ni ghiliba za Wazungu kutaka kuangamiza Waafrika. Lakini Rais Samia akajitokeza na kukaribisha chanjo na yeye kuongoza mamilioni ya Watanzania kuchanja.

Katika miaka hii miwili ya uongozi wake, alikubali kupokea fedha za Shirika la Fedha Duniani (IMF) zilizosaidia kuponya madonda ya UVIKO-19 katika sekta za elimu, afya, miundombinu na nishati.

Madarasa maelfu yamejengwa, vituo vya afya, zahanati na hospitali karibu kila kona ya nchi, ni mambo madogo madogo tu yanayoendelea ili huduma hizo zitolewe kwa ukamilifu.

Tumeshuhudia yote hayo na mengine yakifanywa bila manung'uniko, ikiwa ni pamoja na kuendeleza miradi mikubwa ya kimakakati aliyoianzisha Dk Magufuli kwa gharama kubwa. Ndiyo maana kaulimbiu ya Kazi Iendelee ikazaliwa kutokana na ile ya Hapa Kazi Tu!

Akila kiapo cha kuchukua ofisi hiyo kuu nchini, Rais Samia alisema: "Hakuna litakaloharibika," akiwataka Watanzania kuunganisha taifa lao. "Huu ni wakati wa kusimama pamoja na kuunganika. Ni muda wa kuzika tofauti zetu, kuoneshana mapenzi na kutazama mbele kwa kujiamini.

"Si muda wa kunyoosheana vidole, bali kushikamana na kusonga mbele na kuijenga Tanzania mpya ambayo Magufuli alitarajia kuishuhudia."

Baada ya kauli hii, watu wakasubiri kuona atafanyaje katika nchi hii iliyojawa hofu na kutojiamni kwa baadhi ya watu wakiwamo viongozi waliotumbuliwa muda na saa yoyote.

Lakini kumbe Rais Samia alimaanisha. Mara moja akaandaa mazungumzo ya maridhiano na wapinzani. Hiyo ikiwa ni baada ya kufungulia vyombo vya habari vilivyofungwa, ili kurejesha utulivu katika tasnia hiyo muhimu.

Pia akawa ameruhusu matangazo ya Bunge mbashara kwenye televisheni, ili wananchi kama ilivyokuwa kabla ya utawala wa Magufuli waweze kufuatilia wawakilishi wao nini wanakifanya na nini wanakisema kwa niaba yao.

Ule mwiko wa kusafiri nje kwa kisingizio cha kubana matumizi, akauondoa na yeye kuongoza kwenda nje kuitangaza nchi na kuvuta wawekezaji na watalii, ambao hivi sasa wanafurika kwa wingi kutalii na kutaka kuwekeza. Hatua chanya kwa maendeleo ya nchi.

Kubwa linaloacha alama katika miaka hii miwili ya uongozi wake, ni kuruhusu mikutano ya hadhara ya kisiasa ambayo kwa hakika marufuku yake, iliumiza vichwa wanasiasa wa upinzani. Kwa kweli ilikuwa ni miaka miwili ya kuponya madonda.

# Mbegu za ruzuku za alizeti zadoda

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAKATI msimu wa kilimo cha alizeti ukielekea mwisho, zaidi ya tani 100 za mbegu za ruzuku zilizotolewa na serikali katika mkoa wa Singida hazijawafikia wakulima na ziko mikononi mwa watendaji wa kata na vijiji.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Selestian Choaji, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kwamba ziko halmashauri ambazo zilipewa mbegu za ruzuku za alizeti lakini hazijatumika hadi sasa.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alitoa onyo kwa maofisa kilimo na watendaji wa vijiji na kata ambao wamekaa na mbegu hizo ofisini wakati wakulima wakiwa wanazihitaji kuwa serikali itawachukulia hatua.

"Natoa agizo ifikapo Jumatatu ya kuanzia Machi 20, mwaka huu, mbegu hizo ziwe zimesambazwa kwa wakulima wenye mahitaji vinginevyo halmashauri ilipe fedha za mbegu hizo,"alisema.

Serukamba alisema inashangaza kuona mbegu hizo hazijasambazwa kwa wakulima wakati mkoa uliomba kupatiwa mbegu za alizeti zenye ruzuku ambazo wakulima wangekopeshwa halafu wangelipa wakati wa mavuno kulingana na mahitaji ya kila wilaya.

Alisema halmashauri ambayo inaona haiwezi kutumia mbegu hizo izipeleke katika halmashauri zenye uhitaji vinginevyo zijiandae kulipa.

"Singida tumepata mbegu hizi zenye ruzuku ya serikali, hivyo siko tayari kuona zikiacha kufanyiwa kazi iliyotegemewa. Mkurugenzi wa halmashauri atakayebaki na mbegu hizi lazima alipe," alisema.

Pia Serukamba aliwataka watumishi hasa Maofisa Kilimo kutokaa ofisini badala yake wakawasaidie wakulima na kuhakikisha wanapata mbegu hizo.

Mkoa wa Singida umejiwekea mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ya alizeti hadi kufikia tani 159,110.5 sawa na asilimia 44.2 yanayoingizwa nchini.

Mkakati huo unalenga kuisaidia nchi kuondokana na tatizo la upungufu wa mafuta ya kula na ulianza kutekelezwa katika msimu wa kilimo wa 2021/2022 na ili kufikia malengo hayo umepanga kuongeza eneo la kulima alizeti ambapo zitalimwa ekari 631,391 ambazo matarajio ekari hizo zitazalisha tani 492,485 za alizeti.

# Marekani kumwaga zaidi misaada ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

MAREKANI imeahidi kuendelea kuiunga mkono Tanzania katika jitihada zake za kuimarisha uchumi na maendeleo ya wananchi kwa kutoa fedha na ujuzi mbalimbali pamoja na kuvutia uwekezaji kupitia ubia kati ya sekta za umma na binafsi.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Balozi mpya wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, katika ofisi ndogo za wizara hiyo, jijini Dar es Salaam, alipofika kujitambulisha.

Battle alipongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kusimamia na kukuza uchumi wa nchi na kuamua kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika bajeti yake kwenye sekta za uzalishaji zinazogusa maisha ya watu, kikiwamo kilimo.

"Tunaahidi kuwa Marekani itaendelea kuiunga mkono serikali ya kiongozi shupavu ambaye si tu kwamba anapigania sana maisha ya Watanzania, lakini pia amekuwa mwanadiplomasia anayepigania maendeleo na utangamano wa Afrika," alisema Balozi Battle.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amegusa mioyo ya Wamarekani na viongozi wake ndiyo sababu za Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amepanga kuitembelea Tanzania na viongozi hao wawili watafungua fursa zaidi za ushirikiano wa kiuchumi na kijamii.

Waziri Nchemba aliahidi kufikisha ujumbe wa Balozi kwa Rais Samia na kumwahidi kiongozi huyo kwamba Tanzania iko tayari kutumia fursa za ushirikiano wa nchi hizo mbili kuwahudumia Watanzania.

Aliiomba Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (USAID), kuhakikisha inazipa kipaumbele asasi zisizo za kiserikali (AZAKI) katika utekelezaji wa programu mbalimbali nchini kwa kuzijengea uwezo wa kifedha na kiuendeshaji.

Kuhusu uamuzi wa serikali wa kuzipa kipaumbele sekta za uzalishaji katika mgawo wa fedha za bajeti, Dk. Nchemba alisema sekta hizo zikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi, uendelezaji wa wafanyabiashara wadogo (machinga), utakuza uzalishaji wa mazao, lakini pia kuongeza ajira kwa wananchi hususan vijana.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) Kate Somvongsiri, alimshukuru Dk. Nchemba kwa kutoa hoja ya Taasisi za wazawa zikiwemo AZAKI, kupewa kipaumbele katika miradi inayotekelezwa kupitia Shirika lake hapa nchini.

Alisema utaratibu uliopo hivi sasa ni kwamba asilimia 25 ya rasilimali zinazotumika na shirika lake katika nchi zinaelekezwa kwenye taasisi za wazawa na kwamba kiwango hicho kitaendelea kuongezeka wakati unapowadia kufanya hivyo lakini lengo ni kufika asilimia 50.

Ushirikiano wa Tanzania na Marekani umetimiza zaidi ya miaka 50 na makubaliano ya kwanza ya kuanzishwa kwa uhusiano huo, yalitiwa saini mwaka 1968.




Ofisa Uhusiano wa TTCL, Adeline Berchimance (wa tatu kushoto), kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Mhandisi, Peter Ulanga, akikabidhi sehemu ya msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya wagonjwa wanaopata matibabu katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ya jijini Dar es Salaam jana. Anayepokea kulia ni Muuguzi Msimamizi wa Taasisi hiyo, Mwanga Muhoka. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wapanda miti kutunza vyanzo vya maji

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

OFISI ya Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu (WRBWB) imeanza utaratibu wa kutunza na kuhudumia miche ya miti wanayoipanda ili kuifanya ikue vyema na kuleta maana ya utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji.

Ofisa Misitu Mwandamizi kutoka Bonde la Wami Ruvu, Kitengo cha Kuhifadhi Mazingira, Emmanuel Komba alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Maji huku wakipalilia miti 800 waliyoipanda kwenye ekari tatu, Novemba na Desemba, mwaka jana, pembezoni mwa Bwawa la Mindu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro.

Komba alisema wamelazimika kutunza na kuhudumia miti hiyo ya asili na rafiki katika utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kupalilia na kumwagilia maji kutokana na kuwapo kwa changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa mvua, jua kali na moto unaowashwa bila utaratibu na wakulima.

"Tumepata mwamko wa kutunza na kuhudumia zaidi miti kuanzia sasa katika kuongeza jitihada na juhudi za kufuatilia miti hiyo kwa ukaribu kwa sababu tumeona miti iliyopandwa kipindi cha nyuma haijastawi ilivyotakiwa kutokana na kukabiliwa na magugu na kuathiriwa na moto.

Eneo hili unaloliona lilipandwa miti lakini moto uliopitishwa mwaka jana umeua miti hiyo," alisema.

Alisema kwa kutumia kitalu chenye miche karibu 30,000 kilichoko kwenye ofisi za bonde, watapanda miti mingine zaidi katika eneo hilo na maeneo mengine mvua itakapoanza ili kufanya uhifadhi wa vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira.

Pia alisema katika kutekeleza wiki ya maji yenye kaulimbiu ya 'Kuongeza Kasi ya Mabadiliko Katika Sekta ya Maji kwa Maendeleo Endelevu ya Uchumi', wamejipanga kuongeza kasi katika kutunza vyanzo vya maji ili viwe endelevu.

Alisema ili kukabiliana na changamoto ya mifugo, aliomba serikali kutengea maeneo mengine mifugo ili isiwe na nafasi ya kula miti inayopandwa kwa ajili ya kulinda vyanzo vya maji.

Komba alisema ni jukumu la kila mwananchi kulinda maeneo ya vyanzo vya maji sababu vyanzo hivyo lazima vitunzwe huku jukumu hilo likiwa la kila mtu nchini kwa sababu maji hayana mbadala kwa kila mmoja. Kaimu Mkurugenzi Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Elibariki Mmasi, alisema suala la kutunza na kuhudumia miti iliyopandwa ni endelevu kwa sasa nchini ili kuboresha vyanzo vya maji na kuepuka kurudiarudia kupanda miti katika maeneo yale yale jambo linalosababisha usumbufu na hasara pia kwa serikali.

Maadhimisho ya Wiki ya Maji duniani yalianza rasmi Machi 16, mwaka huu, na yanatarajiwa kukamilika Machi 22. Kitaifa yanafanyika jijini Dar es Salaam.

# MAISHA

MACHI 19, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Nyama duara zinavutia

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Tengeneza eneo la chakula kwa nafasi ya nyumba yako




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# Urembo Uliokamilika

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | U | A | ■ | M | B | A |
| A | ■ | ■ | ■ | B | ■ | N |
| N | ■ | T | U | A | ■ | G |
| D | A | I | ■ | T | A | A |
| I | ■ | M | I | A | ■ | Z |
| K | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| A | R | A | ■ | S | A | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BAI, DUA, AKA, JUA, GOA, TAI, MIA, POA, INGIZWA, MAPYA, BWATA, JENGEWA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

1. AMIJ
2. CAHI
3. ODSA
4. ISJIU
5. KAWHAA
6. AMZIAW




## WATOTO

# PAKA RANGI




### CHEKA

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama kokonono wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora ununulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**

Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Uovu uliotendwa na wazazi unatesa watu wengi hivi leo

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilianza na mada iliyohusu misingi mibaya inavyozima ndoto za watu wengi. Bado naendelea kukazia eneo hilo kutokana na uzito wake katika jamii yetu.

Maisha mazuri ya mtu husababishwa na misingi yake mizuri. Maandiko ya Mungu yanaweka vizuri jambo hili pale neno linaposema, "misingi ikiharibika, mwenye haki atafanya nini?"

Kumbe kuna misingi iliyoharibika. Wako watu vile walivyo ni kwa sababu ya misingi yao mibovu. Misingi yao ni mibaya, chanzo chao ni kibaya. Haiwezekani mtu akasomeshwa na fedha za wizi, fedha za dhuluma halafu baadaye akawa na hatma nzuri. Hapana!

Baba yako alidhulumu kabisa, akauza shamba la watu akapewa fedha akakupeleka wewe shuleni. Umesoma kwa pesa zinazonuka damu za watu. Huwezi ukawa na maisha mazuri. Yakupasa urudi nyuma misingi yako inasemaje?

Kule kwenu kukoje, kwa baba yako kukoje, kwa mama yako kukoje? Hao wazazi wako walikuwaje? Walikuwa wakitenda matendo gani? Babu yako alikuwa akiamini katika nini? Waliabudu kitu gani na leo wanafanya nini? Wako wapi, wanaamini nini?

Chimbuko lako linasemaje? Wakati unazaliwa nani alikupokea? Kitovu chako walikiweka wapi na nywele zako za utoto walizipeleka wapi? Hivyo ni vitu ambavyo unapaswa kuvifanyia utafiti wa kiroho. Kwamba hivi vitu vilikwenda wapi?

Unafanya bidii lakini matokeo kidogo. Unashika pesa lakini hazikai. Lazima urudi ndani katika maisha yako. Ukiona hivyo unapaswa kufanya utafiti kwanza wa kimwili kwamba mbona nafanya kazi lakini sifanikiwi, mbona sitoboi? Baada ya hapo, unaanza utafiti wa kiroho. Unachunguza, hivi kule kwetu ni nani aliyefanikiwa, ni nani aliyesoma, nani ana hela nyingi, nani ana maisha mazuri ya furaha?

Rudi fanya utafiti, kwenye familia yenu, nani anaoa au wanaolewa? Na je, kuna anayedumu kwenye ndoa? Lazima uanze kuchunguza, mama aliolewa na wanaume wangapi, baba alioa wanawake wangapi. Babu je, alikuwa na wake wangapi?

Si ajabu ukajikuta kwenye kifungo hicho. Katika ulimwengu wa mwili utaona mambo yako sawa lakini wakati utafika mambo yataanza kuharibika. Zile roho zitaanza kuonekana.

Ukitafiti utagundua kama baba au mama yako alikuwa vile na huenda nawe yakakukuta. Kwa hiyo unatakiwa kuanza kukata mawasiliano kwa maombi. Lazima ukatae yaliyowakuta wazazi wako yasije kwako na uzao wako.

Huwezi kupigana vita na mtu usiyemjua. Kuna jambo lazima ulifanyie utafiti. Neno la Mungu linasema, "Na watu wa kwenu watakaobaki watafifia kwa ajili ya uovu wao, kwa hizo nchi za adui zenu; tena watafifia kwa ajili ya uovu wa baba zao."(Walawi 26: 39). Unaweza usiendelee kwa sababu ya uovu wa baba yako!

Kumbe uovu wa baba yako unaweza kusababisha maisha yako yasistawi. Au uovu wa mama yako unaweza ukakudhuru wewe. Unajaribu kufanya vitu haviendi, biashara huoni faida, ni hasara tu.

Watu hawakupendi, kumbe kuna uovu wa baba au mama yako umesimama kukuzuia usipenye. Unamwomba Mungu kwa machozi, unagaragara kwa magoti lakini wapi. Kumbe kuna uovu wa wazazi wako unakutesa.

Unaamua kufunga kwa kujinyima chakula siku saba, siku 21, siku 40 lakini huoni matokeo. Kumbe kuna shida mahali, ishughulikie. Walokole wengi hawajui wanapambana sana, Utalalamika mbona inzi wananifuata. Lazima ujichunguze kwa nini wanakufuata, lazima kuna kamzoga mahali.

Shughulika na huo mzoga, uutupe. Mtu unalalamika mbona watu wananichukia. Lazima ujichunguze kwani lazima iko sababu si bure. Laana haimpati mtu bila sababu. Ukiona mtu amepata laana lazima iko sababu.

Mtu atasema kwa nini mimi siolewi au sipati mchumba wa kuoa. Wale walio wadogo kiumri na mimi wanaoa mimi niko pale pale na umri umeenda sana.

Nina mkosi gani? Kumbe unapaswa kurudi kwenye misingi ya kwenu.

Ukiona mambo hayaendi shituka mapema usingojee mambo yaharibike ndipo uchukue hatua. Mungu alishaweka maelekezo, sheria na amri zake na tusipozifuata hawezi kufanya lolote.

Jiulize ni vazi gani umevaa linalozuia mafanikio yako. Ushirikina au uzinzi? Au bado unafanya matambiko na kuabudu mizimu, mambo ambayo ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu? Jitafakari!

**Tutaendelea wiki ijayo. Una kisa, maoni? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kataa utamaduni wa magharibi unaotweza utu

Vita vinavyoendelea nchini hivi sasa vya ukatili wa kingono hasa ulawiti dhidi ya watoto, ushoga, usagaji au kwa jina lingine mapenzi ya jinsia moja, ni masuala yanayochochewa na mabadiliko ya kijenetiki, ambayo huchochea tabia ya kutweza utu.

Leo, sitajikita kuzungumzia kwa undani aina za utu yaani 'introvert', 'extrovert' na 'ambivert'. Badala yake, kwa ufupi sana, nitajikita kujadili aina hii ya 'ambivert', ambayo inatumiwa sana na watu hawa tunaowakataa katika jamii kutokana na hulka yao na mienendo yao katika kuharibu taifa la Mungu.

Kwa namna Watanzania na baadhi ya waafrika wenzetu wanavyopambana kukataa mapenzi ya jinsia moja, ni dhahiri kwamba hawajakosea, kwa kuwa wanapata msukumo mkubwa wa kiimani wa kupingana na mashoga na mabasha, kupitia maandiko matakatifu yaliyoko kwenye Biblia katika kitabu cha Warumi 6: 6-13.

Katika kitabu hicho imeandikwa: "Mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi."

Aidha, kitabu hicho kimeandika, "wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki."

Yamkini, kugunduliwa kuchomoza matukio yanayotweza utu wa binadamu, hasa kwetu Watanzania, wako watu waliojitoa mstari wa mbele kupinga kwa nguvu, mapenzi ya jinsia moja.

Bravo! serikali ya Rais, Samia Suluhu Hassan, imekuwa mstari wa mbele wakati wote kukataa utamaduni huu. Wanaharakati na baadhi ya viongozi wa dini, ninyi ni Simba wa vita, anzeni kazi.

Wanasiasa siwasikii katika vita hii, sijui au kwa kuwa ni wapiga kura? tuongeze nguvu kulaani na kupiga vita utamaduni huu usiote mizizi katika taifa letu.

Iko haja kama taifa, kuwa na mkakati wa pamoja wa kupambana na tamaduni za kigeni zinazotweza utu. Ifike mahali tuwe wakali na kutumia sheria zetu kuwaadhibu wanaoendekeza vitendo vya ushoga, mabasha na wasagaji, kama tunavyozitumia sheria hizo hizo kuwafunga miaka 30 jela au kifungo cha maisha jela, wanaotiwa hatiani kwa makosa ya ulawiti, ubakaji au unajisi.

Tunayo Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2022; ni wakati muafaka kama taifa, mahakama zetu na vyombo vyetu vitumie sheria hii kubana wahusika wa matendo yanayotweza utu wa mwanadamu ili wajue ni makosa.

Iko hivi! hata kukubali tu kuingiliwa kinyume na maumbile, ni kosa na ni kinyume na kifungu 154 (1) (c) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria iliyofanyiwa Marejeo ya Mwaka 2022.

Laiti wangelijua kwamba utu unaweza kueleweka kama seti ya mara kwa mara ya sifa mbalimbali za kisaikolojia na mambo mbalimbali ya ndani, ambayo huathiri tabia ya binadamu, wasingefanya haya!

Hata kama hawajui kwamba utu ni njia ya kufikiri, tabia na hisia, lakini itoshe kusema kwamba kuna nadharia nyingi juu ya kile kinachoathiri malezi yetu, utu, licha ya kwamba watu wengine huzingatia jeni.

Hata hivyo, kwa kuwa si pekee inayoamua tutakuwa watu wa aina gani, ushawishi juu ya maendeleo ya utu pengine unatokana na mazingira yanayotuzunguka, yaani nyumba ambayo tunalelewa, watu wa karibu sana, mawasiliano na wenzetu na mambo mengine mengi.

Kwa jinsi tulivyo, masuala haya yanaweza pia kuwa yanatokana na kuathiriwa na muundo na utendaji wa mfumo wa neva. Linaweza pia kuwa tatizo la kihomoni.

Ni lazima Watanzania wajue kwamba, utu ni mchakato wa muda mrefu, ambao huanza na kuzaliwa na kuendelea katika utoto hadi ukubwani. Kwa sababu utu una jukumu muhimu sana katika tabia ya binadamu, tukatae tamaduni za magharibi zinazotweza utu!

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

**Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

**Simu ya mkononi: +255 767 535490**

## HARUSI






Ilikuwa siku ya furaha kwa Fakhi Athumani baada ya kuamua kula kiapo cha ndoa na mkewe Khadija Ngonyani, katika harusi iliyofungwa Machi 4, mwaka huu eneo la Vikindu Chatembo, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.






# MITINDO









# USIKU WA IRADA STYLE

## Ulivyong'arisha mavazi ya kistaarabu

KILELE cha maonyesho ya mavazi ya stara kimetikisa jiji la Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana, baada ya watu waliohudhuria kupagawa kutokana na umahiri wa ubunifu wa mitindo iliyoonyeshwa jukwaani.

Usiku huo ulikuwa maalum kwa mbunifu anayekuja kwa kasi Irada Mtonga anayemiliki lebo ya Irada Style, kuonyesha kazi zake mbalimbali katika kutimiza miaka mitano tangu aingie katika tasnia hiyo.

Katika maonyesho hayo ambayo yalihudhuriwa na wanawake kutoka tasnia mbalimbali, mgeni rasmi alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Tanga mjini, Dalmia Mikaya. Alipojitokeza jukwaani kwa mara ya kwanza, Irada alipokelewa kwa shangwe huku akiambatana na wanamitindo waliovalia nguo alizobuni mwenyewe.

Wakati akiwashukuru watu waliokwenda kuhudhuria maonyesho hayo. Alisema lengo la maonyesho hayo ya mavazi ni kutoa ujumbe kwa wanawake kuwa wana uhuru wa kuvaa kile wanachopenda, lakini wasiende kinyume na ustaarabu wao.

"Maonyesho haya ya mavazi si kwa ajili ya kuonyesha mitindo ya nguo, bali nataka kuwaambia wanawake tuna uhuru wa kuchagua nini tuvae bila kuondoa ustaarabu na utu," alisema.

Katibu Tawala, Mikaya, alimpongeza mbunifu huyo kwa kazi nzuri aliyoonyesha jukwaani na kwamba serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, inajivunia kuwa na wajasiriamali kama yeye.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# UREMBO ULIOKAMILIKA



## Uso bila sunzua unang'aa

MATATIZO ya ngozi hutofautiana kuanzia kwa dalili na ukali wa athari zake.

Baadhi ya watu huwa na athari ya muda au ya kudumu ilhali mengine hutoweka baada ya muda mchache.

Sunzua ni nyama zinazoota juu ya ngozi ambazo zinaweza kutokea usoni, kuzunguka jicho, shingo, mgongoni na kadhalika.

Sunzua ni vinyama vyeusi ambavyo husababishwa na matatizo ya homoni wakati wa ujauzito au unene kupita kiasi.

Matibabu yake hufanyika hospitalini kwa kutolewa na vifaa maalumu.

Pia unaweza kutibu nyumbani kwa njia za asili.

Kitunguu saumu

Kiponde alafu paka maji yake juu ya kisunzua. Njia hii inaondoa haraka kisunzua ila inauma.

Pia jitahidi maji ya kitunguu saumu yasiguse ngozi kwani yanaunguza. Paka mara mbili kwa siku.

Kiazi mviringo

Kioshe kiazi halafu kikate kiwe vipande vidogo kisha paka maji yake juu ya kisunzua. Sugua kwa kutumia kipande cha kiazi.

Kitunguu maji

Kikate halafu sugua juu ya sunzua.

Limau

Kata limau kisha sugua juu ya sunzua ikiwa na maji.

Uzi

Kama sunzua ni kubwa unaweza kutumia uzi. Loweka uzi kwenye maji ya limau au kitunguu, kisha kifunge mara kwa mara.

Njia nyingine ni rangi ya kucha, siki ya apple cider na ganda la ndizi mbivu.

Njia zote hizi, tumia mara mbili kwa siku. Unaweza kuona kama havitoki ila baada ya mwezi vitaondoka.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Nyama duara zinavutia

NYAMA ya duara ni aina ya mboga nzuri sana, watu wengi hawajui kuitengeneza.

Hata hivyo, leo tutaelekezana ili kila mmoja afaidi chakula hiki kitamu.

Kilo moja ya nyama ya kusaga ya ng'ombe au nyama nyingine, kikombe cha karoti nusu, vitunguu maji viwili, mayai, limao au ndimu moja, tangawizi moja, kijiko kimoja cha kiungo cha majani ya Italian, chumvi kiasi na kitunguu saumu kimoja.

Namna ya kuandaa

Andaa viungo vizuri kwa kukata karoti na vitunguu. Hakikisha ziwe nyembamba.

Andaa nyama yako ya kusaga kwenye chombo, changanya viungo vyote kwa pamoja na Koroga vizuri upate mchanganyiko unaofaa.

Baada ya muda, weka nyama kwenye viungo,unaweza kuongeza viungo unavyopenda, upande wangu napendelea maggie, tangawizi na kunyunyuzia limao au ndimu kwa mbali.

Finyanga mabonge vizuri ya nyama. Unaweza kutumia kijiko ili kupata umbo zuri zaidi. Rudia zoezi hili hadi nyama yote iishe.

Weka chungu jikoni kisha weka mafuta ya kula na acha yapate moto vizuri.

Chungu kikiwa tayari, weka nyama na pika hadi ziive vizuri. Hakikisha zimeiva na angalia kama hazina rangi ya pinki kwa ndani. Endelea kupika kwa dakika 5 kama bado hazijaiva.


Rudia hadi umalize zoezi la kupika nyama zote, weka kwenye mfuko wa nailoni na ziweke kwenye friji au jokofu na uache kwa muda wa siku 2 au zaidi.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Tengeneza eneo la chakula kwa nafasi ya nyumba yako



ASILIMIA kubwa ya wamiliki wa nyumba hujali sana kuwekeza nguvu zao katika sebule.

Naamini kwamba wengi wanafanya hivyo kwa sababu ndiyo sehemu inayotumika sana katika kuketi wageni na kufanyia mazungumzo mbalimbali.

Pamoja na umuhimu huo, leo nataka tugeukie upande mwingine wa eneo linalotumika kwa chakula (dining room) ambalo pia nalo ni muhimu.

Katika nyumba nyingi, chumba hiki huwa kimetazamana na sebule japokuwa wachache hukitenga na ukuta, hivyo kinakuwa hakionekani.

Tuanze na kwa hawa ambao chumba hiki kinachotumika kwa chakula kinaonekana. Hapa nataka tujifunze



kwanza ni namna gani tunahitaji kiwe, nini kinapaswa kukaa humo na kitu gani hakipaswi kukaa.

Na kama hakijakaa vizuri ni namna gani unataka kiwe kulingana na vile unavyo 'design' wewe. Pia kumbuka kabla ya kuweka kitu chochote, hakikisha unaangalia kwa nafasi iliyopo katika chumba chako hicho.

Baadhi yetu tumezoea kwamba 'dining' lazima kwanza iwe na meza kubwa au ndefu. Si lazima uwe na meza refu, isipokuwa unachopaswa kuzingatia ni nafasi iliyopo katika chumba hicho na uzingatiaji katika 'desining'.

Ukishajua namna ambavyo unataka kupangilia chumba chako hicho, hapo ndipo unaweza kuamua au kupaka rangi kwa kuzingatia isipishane sana na ile iliyopo sebuleni au iwe katika kundi hilo na hiyo ni kwa chumba cha chakula kinachotazamana na sebuleni.



## Maua yanayoweza kuongeza hewa safi

**Na Restuta James**

MABADILIKO ya tabianchi na uchafuzi wa hewa unaotokana na moshi wa viwandani pamoja na wa magari ni jambo lisilokwepeka hususani kwa wakazi wa mijini.

Hii ni kwa sababu makazi ya watu yapo karibu na viwanda na hata yaliyo mbali hayawezi kukwepa uchafuzi unaosababishwa na uwekezaji huo.

Katika makala ya leo, tunakuletea maua yanayoweza 'kusafisha' hewa, rahisi kupatikana na kuyatunza pia.

Katika orodha hii, mengi ya maua haya yanahitaji jua au mwanga mdogo na maji kidogo pia. Kwa wale ambao wanakabiliwa na shida ya maji hawana sababu ya kukosa maua kwenye vibaraza vyao kwa kuwa hayahitaji eneo kubwa wala maji mengi.

1. Snake plant au ulimi wa mama mkwe

Ulimi wa mama mkwe ni ua muhimu sana kutokana na upekee wake katika kuongeza hewa safi ya oksjeni na kusafisha hewa kwa ujumla.

Wataalam wa mimea wanaeleza kuwa ni ua lenye faida nyingi za kiafya ambalo linaweza kuwekwa katika chumba cha kulala kutokana na uwezo wake wa kubadili hewa ya kabonidayoksaidi kuwa oksjeni nyakati za usiku.


Hii ni tofauti na mimea mingine mingi ambayo nyakati za usiku huzalisha hewa chafu badala ya oksjeni kama inavyofanya mchana.

Wataalam wa mimea wanalitaja kama chujio la hewa ya ndani ya nyumba linaloweza kuimarisha afya ya akili hasa likiwekwa chumbani.

Watu wengi wanapenda kuliweka kibarazani na katika maofisi huwekwa eneo la mapokezi. Wataalam hao wanaeleza kuwa ni zuri sana likiwekwa chooni na vyumbani.

Wiki ijayo itakuletea orodha ya maua haya ambayo yanapatikana nchini nzima

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
...KIANGAZI...
SUBIRINI MASIKA MTARO UZIBE MPATE AKILI VIZURI.
USITUPE TAKA AMRI
ETI JITU LIMEFIKA HADI KWA MKEWE LINARUDI ETI LINADAI JERO CHENJI YAKE!
BAR
MGANGA UNA-NIKUMBUKA?
NAJIBU KWA HELA
NINGELAZIMISHWA NINGELIFUNGA JITU, SIO KWA 'TUNGI' HILI!
ALOKWAMBIA KAZI HOTELINI HAINAGA BONAS' NAN KASEMA!
SEMBE
HOMU
SASA HII NDIO GARI GANI HUKU KIJIJINI?
UNAHAMU UROGWE!
BEBI NISINDIKIZE NAOGOPA KUKABWA!
MKABAJI ATAKUWA KAJIFUNZA KUMKABA 'TEMBO'
BABA MWENYE NYUMBA UTAKUWA WEWE BHANA!
SASA RUDI UME-LEWA WAKATI MIMI NNA KIU!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...YAKIKUKUTA NDIO UTAJUA UMUHIMU WA MBIO...

# ICC yatoa kibali cha kumkamata Rais Putin

**THE HAGUE,** UHOLANZI

MAHAKAMA ya Kimataifa yenye kuhusika na makosa ya jinai (ICC) imetoa waranti ya kukamatwa kwa Rais wa Russia, Vladimir Putin kutokana na uhalifu wa kivita.

Pia imemtuhumu kwa uwajibikaji wa kibinafsi kwa utekaji nyara wa watoto nchini Ukraine.

Hatua hiyo ni ya kwanza kutokea kwa mahakama hiyo kutoa hati ya kukamatwa dhidi ya mmoja wa viongozi wa mataifa wanachama watano wa kudumu wa baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Katika taarifa yake ICC, ilisema Rais Putin anadaiwa kuwajibika na uhalifu wa kivita kwa kufanya uhamisho haramu wa watoto kutoka maeneo waliyoyanyakua ndani ya Ukraine.

Mahakama hiyo pia imetoa hati ya kukamatwa kwa Maria Lvova-Belova, kamishna wa Haki za Watoto katika Ofisi ya Rais wa Russia.

Mwezi Oktoba Shirika la habari la AP, liliandika ripoti kuhusu kuhusika kwa kiongozi huyo katika kuwateka watoto yatima wa Kiukraine.

Uchunguzi huo ulikuwa wa mwanzo, ambao ulifuatiliwa hadi ndani ya Russia kwa kukusanya ushahidi kadhaa.

Hatua hiyo, Russia imeipuuza, lakini ilipokelewa kwa furaha na Ukraine.

Licha ya kutolewa kwa hati hiyo, matokeo yake yanaonekana kuwa madogo kwa Rais Putin kupanda kizimbani mjini The Hague kwa kuwa serikali ya Russia haiitambui kisheria mamlaka ya mahakama hiyo.

Adil Ahmad ambae ni mchambuzi katika sheria za kimataifa, alisema Putin anaweza kwenda China, Syria, Iran na kwa washirika wake wachache, lakini hawezi kwenda katika maeneo mengine.

David Crane, mwendesha mashtaka wa kimataifa wa zamani, aliliambia shirika la habari la AP kwamba Vladimir Putin anatazamwa kama mtu aliyepoteza uaminifu wake kisiasa duniani.

Kupitia taarifa yake kwa njia ya video, Rais wa Mahakama ya ICC, Piotr Hofmanski alisema majaji wa mahakama hiyo wametoa waranti, lakini litakuwa jukumu la jumuiya ya kimataifa kuitekeleza.

Mahakama hiyo haina polisi wake ambao wanaweza kulisimamia zoezi hilo.

Katika hatua nyingine, Rais wa Marekani Joe Biden, amepongeza uamuzi wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), kutoa hati ya kukamatwa kwa kiongozi huyo wa Russia.

Putin ni rais wa tatu kupewa hati ya kukamatwa na mahakama ya ICC.

Rais Biden alisema kuwa, wakati mahakama haikuwa na mamlaka yoyote nchini Marekani, lakini utoaji wa kibali hicho unaleta maana kubwa.

Utawala wake ulikuwa tayari umeamua kutambua Russia imefanya uhalifu wa kivita wakati wa mzozo unaoendelea nchini Ukraine.

Makamu wa Rais, Kamala Harris, aliwahi kusema kwamba wale waliohusika watawajibishwa.

Umoja wa Mataifa pia ulitoa ripoti mapema wiki hii ambayo iligundua kitendo cha Russia kuwaondoa watoto wa Ukraine kwa lazima na kuwapeleka katika maeneo yaliyo chini ya udhibiti wake na kutambua hilo kuwa sawa na uhalifu wa kivita.

**DW**

## Trump arudishwa kutumia You Tube

**WASHINGTON,** MAREKANI

MTANDAO wa kijamii wa YouTube umerejesha akaunti ya aliyekuwa rais wa Marekani, Donald Trump, baada ya kusimamishwa kwa miaka miwili kwenye jukwaa hilo.

Hatua hiyo inafuatia maamuzi sawa yaliyochukuliwa na kampuni ya Meta, ambayo inamiliki mitandao ya Facebook na Instagram, na Twitter inayomilikiwa na Elon Musk.

Kiongozi huyo alipigwa marufuku kuchapisha video za YouTube mnamo Januari 2021, huku YouTube ikisema wakati huo kuwa chaneli yake ilikuwa imekiuka sheria zake kuhusu uchochezi wa ghasia.

Lakini akaunti yake sasa imerejea mtandaoni, hayo ni kulingana na akaunti ya wanahabari ya YouTube.

“Kuanzia leo, chaneli ya Donald J. Trump haijazuiliwa tena na inaweza kupakia maudhui mapya,” YouTube inayomilikiwa na Google iliandika kwenye Twitter.

“Tulitathmini kwa makini hatari inayoendelea ya vurugu za ulimwengu halisi, huku tukisawazisha nafasi kwa wapiga kura kusikia kwa usawa kutoka kwa wagombea wakuu wa kitaifa kabla ya uchaguzi’” alieleza.

“Chaneli hii itaendelea kuwa chini ya sera zetu, kama ilivyo kwa njia yoyote. kituo kingine kwenye YouTube.” Taarifa hiyo ilisisitiza.

Hata hivyo, upande wa Trump, haujazungumza chochote kuhusu uamuzi huo, licha ya awali kulalamikia hatua zilizochukuliwa za kumuondoa katika mitandao ya kijamii.



Wafuasi wa Waziri Mkuu wa zamani wa Pakistan, Imran Khan, wakikusanyika nje ya makazi yake kupinga polisi kumkamata ndani ya nyumba yake mjini Lahore hivi karibuni. **PICHA: EPA-EFE**

# Wanigeria kuwachagua magavana

**ABUJA,** NIGERIA

RAIA wa Nigeria wamerudi tena katika masanduku ya kura katika uchaguzi wa kuwachagua magavana katika majimbo 28 kati ya 36 ya nchi hiyo. Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi, ilisema zaidi ya wagombea 800 wanawania nyadhifa za ugavana katika majimbo hayo.

Macho yote yatakuwa kwenye kinyang’anyiro cha kutawala kitovu cha kibiashara, cha Lagos, jimbo analotoka Rais mteule Bola Tinubu.

Peter Obi wa chama cha upinzani cha Labour alimshinda Tinubu eneo hilo katika kinyang’anyiro cha urais.

Kano, jimbo kubwa zaidi kaskazini mwa Nigeria na jimbo la Rivers katika eneo lenye mafuta la Niger Delta yako chini ya ulinzi.

Lakini kuna wasiwasi wa kiusalama katika eneo la kaskazini mashariki ambako makundi ya waasi yamekuwa yakifanya mashambulizi ya mara kwa mara.

Katika eneo la kusini mashariki, shughuli za waasi wanaotaka kujitenga pia zimezua hofu ya kutokea vurugu.

Kufuatia mashambulizi wakati wa uchaguzi, vikosi vya usalama vimetumwa kwa wingi katika baadhi ya maeneo ya nchi hiyo.

Wakati huo huo, Inspekta Jenerali wa Polisi wa Nigeria alitangaza kupiga marufuku harakati zote za magari katika majimbo yaliyoathiriwa, kuanzia saa sita usiku wa Ijumaa hadi saa 12:00 Jumamosi.

Magavana wa majimbo wana nguvu kubwa nchini Nigeria.

Pia inasemekana kuwa baadhi ya wanasiasa huwapa silaha majambazi katika jitihada za kutaka kushinda kwa gharama yoyote ile.

**BBC**

MAKALA

# KILIMO NI UCHUMI, TUKIFANYE KWA VITENDO



Na Magabilo Masambu

MSINGI wa uchumi wa nchi yetu ni kilimo na, hilo halina ubishi. Bahati mbaya tuliyo nayo ni uwekezaji hafifu katika eneo hili ambalo linaajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

Jambo la kilimo limesalia kama chaguo la watu walioshindwa shughuli nyingine zote ndiyo wanasema pengine jaribu kilimo.

Mataifa makubwa duniani kabla ya viwanda, yalianza kuweka nguvu kubwa katika kilimo kwa sababu malighafi nyingi za viwandani hutokana na kilimo. Mapinduzi ya viwanda Marekani na Ulaya yalihitaji malighafi ndiyo maana ikasababisha kuwapo na biashara ya utumwa hasa barani Afrika.

Sasa kama Marekani na Ulaya waliendelea kwa kutumia malighafi zetu kutoka Afrika, kwa nini sisi tunashindwa kuzitumia ili tuendelee? Wako watakaosema hatuna viwanda, ndiyo tutakuwaje na viwanda wakati hatuzalishi malighafi zitakazochochea uanzishwaji wa viwanda?

Kama tunataka nchi hii ipige hatua kimaendeleo, lazima suala la kilimo lisiwe la mtu mmoja mmoja uwe ni mkakati wa kitaifa ambao unasimamiwa na serikali. Natambua kuna juhudi mbalimbali zinachukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo lakini miaka nenda rudi imekuwa michakato, mipango, mikakati bila mafanikio katika sekta ambayo ndiyo iliyobeba watu wengi. Tukiacha michakato tukaamua kwa dhati kufanya uzalishaji wa chakula cha kutosha, hutasikia watu wanailalamikia serikali juu ya ajira maana wanaolalamika wote wana njaa ya chakula na kwa sababu hawana ajira, hawana mtaji wa kuweka kwenye kilimo.

Kuongoza taifa la watu wenye njaa si kazi rahisi. Kuwafanya watu wenye njaa washibe ni jambo rahisi kama kuna nia ya dhati katika kuhakikisha nchi inakuwa na chakula cha kutosha. Hizi hadithi za kila siku kusingizia ukosefu wa mvua katika karne hii ya sayansi na teknolojia hatutakuwa tofauti na kilimo kilichokuwa kinafanyika nyakati za ujima. Tunapaswa kuonyesha huko tumeshatoka na sasa tunaweza kuishi bila kutoa visingizio vya mvua wakati kila kona ya nchi tumezungukwa na vyanzo vya maji.

Nchi kama Libya iliwezaje kufanya kilimo cha umwagiliaji wakati karibu nchi yote ni jangwa? Sisi tunakwama wapi? Sababu za kushindwa kwa kilimo kila mwaka zimekuwa zile zile.

Tunawezaje kutoka hapa tulipo ili tusogee mbele na tuwe tofauti na miaka ya ujima? Nafikiri ni muhimu serikali pamoja na wadau mbalimbali kuweka nguvu ya pamoja kuhakikisha mazingira yanakuwa rafiki ili wananchi tuweze kuzalisha chakula cha kutosha kisichotegemea mvua.

Najaribu kufikiri hivi siku mvua ikigoma kabisa angalau kwa miaka hata mitatu mfululizo tutafanyaje? Maana kwakweli lazima tuwapongeze wakulima wachache wanaotuokoa kwa kutumia kilimo hiki cha jembe la mkono pamoja na kwamba wanalima kutafuta kujikimu lakini wanalisaidia sana taifa kuepukana na njaa kali kwahiyo ingekuwa jambo la busara zaidi kuwatengenezea mazingira ili wazalishe zaidi wauze ndani na nje ya nchi.

Tunaposema kilimo ni uchumi maana yake hakuna uchumi bila kilimo, hakuna mtu atafanya kazi nyingine za uzalishaji bila kwanza kuwa na chakula, hatutaishi duniani bila chakula lakini tunaweza kuishi bila mambo mengine. Kuvaa siyo lazima japo ni muhimu lakini kula si muhimu tu ni lazima kwahiyo ndiyo kusema anayefanya biashara ya chakula anao wateja zaidi na wa uhakika kuliko anayefanya biashara za nguo na kama ndivyo kwanini tusitengeneze mazingira ya biashara ambayo tayari inaowateja wa uhakika?

Inafika mahala eti tunafikiria kufunga mipaka ili chakula kisitoke, yaani tunayo fursa ya kutosha kuuza bidhaa badala ya kuzalisha zaidi ili tushindane na soko la uhakika na watanzania wainuke kiuchumi tunafikiria kufunga mipaka.

Tuzalishe zaidi ili tuuze zaidi nchi na mtu mmojammoja ajipatie kipato. Tuachane kabisa na suala la kutegemea kilimo cha mvua, yaani iwe kama mvua ipo tunashukuru kama haipo tuwe na njia mbadala za kufanya uzalishaji.

Hatuhitaji kulima nchi nzima tunahitaji kuainisha maeneo ambayo ni rafiki katika kilimo cha umwagiliaji, kisha maeneo hayo machache yalishe nchi nzima tukijumlisha na kilimo cha mvua katika maeneo ambayo si rafiki katika umwagiliaji nchi nzima itakuwa na chakula cha kutosha na ziada na hivyo kelele za hatuna ajira sijui vyuma vimekaza, vyuma vitalegea kwasababu sasa watu wanachakupeleka kinywani.

Maisha yanakuwa magumu si kwa sababu ya watu kukosa fedha bali watu kukosa chakula, sasa ikitokea hawana chakula na hawana pesa tabu inakuwa maradufu, lazima kwa vyovyote vile maisha yawe magumu kupindukia.

Wakati tunakua fedha hazikuwa na matumizi sana, kwasababu suala la chakula halikuwa tatizo kutokana na hali ya uzalishaji uliotokana na hali nzuri ya hali ya hewa na rutuba japo kuna vipindi vichache vichache palijitokeza njaa ya kutisha kwenye baadhi ya maeneo ya nchi.

Tunaelekea kwenye mvua za masika na kwasababu bado tunategemea kilimo cha mvua, basi twendeni mashambani angalau tufanye kilimo cha mazao ya muda mfupi kama maharage au mahidi ya muda mfupi angalau baada ya mavuno huko mbeleni, tupunguze gharama kubwa za vyakula sokoni na pengine kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Ashura aliyedanganywa kwa chipsi mayai, bia, kuku, yakabaki majuto*



Na Adam Fungamwango

RAIS wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Kikwete, alishawahi kutoa msemo mmoja ambao ukawa maarufu sana. Na ni maarufu hata leo, likiwa linatokea jambo kama hilo.

Msemo huo ni 'Akili za kuambiwa changanya na zako.' Alikuwa na maana kwamba lolote utakaloambiwa kwenye hii dunia, usikurupuke kulifanya bila wewe mwenyewe kulifanyia tathmini.

Mifano ipo mingi sana na kuna baadhi ya wafanyakazi ambao baada ya kupata pesa, ziwe za mkopo au hata za kustaafu waliambiwa na rafiki zao wafanye biashara fulani. Wakahakikishiwa kuwa inalipa na watapata faida nyingi. Kuna walioingia kichwakichwa na kufanya biashara waliyoambiwa ambazo hawajawahi kuzifanya tangu kuzaliwa na hawana hata uzoefu nazo na hawajui mzunguko na mlolongo wake unakuwaje. Wakajikuta wanakata mtaji na hakuna chochote kilichofanikiwa zaidi ya madeni, kilio na kusaga meno.

Kama wangeamua kuchanganya na akili zao, kuanza uchunguzi wa jinsi biashara hizo zinavyofanyika, mzigo unanunuliwa wapi, unasafirishwa vipi, gharama yake inakuwaje, unauzwa bei gani na faida yake ni kiasi gani pengine wasingepata shida waliyoipata.

Kwenye dunia hii kuna watu waongo na walaghai. Ni lazima uwe makini sana kuchuja maneno, ushawishi au ahadi wanazotoa.

Hata kwenye nyanja ya mapenzi, huko kuna ulaghai wa 'kufa mtu.' Wakati wanaume wanawaona wanawake ni waongo, wanaume hawajijui kama wao ni walaghai wakubwa. Mwanamke anaweza kumwongopea mwanamume kwa kumpa ahadi halafu asiitimize. Akajifanya anaumwa ili atumiwe pesa, lakini kumbe ni ya matumizi mengine na uongo mwingine mwingi ambao kwa asilimia kubwa hauathiri mwenendo na maisha ya mwanaume.

Lakini ulaghai wa wanaume umewasababishia matatizo makubwa wanawake. Umewafanya kuachana na wapenzi wao wanaowapenda kwa dhati na kuangukia mikononi mwa mafedhuli.

Wamewaacha waume zao wanaowathamini licha ya mapungufu ya hapa na pale, wakakimbilia kwa wanaume mabedui ambao wao wanatamani zaidi kuliko kupenda. Siku mbili tatu tu anamchoka na kumtimua. Hajali kama alimlaghai akatoka kwa mwanamume mwingine au kwenye ndoa.

Hajali aibu atakayoipata akimrudia kumlamba miguu mumewe amrudie. Kusema kweli ni ukatili wa kijinsia. Pamoja na hayo, baadhi ya wanawake pia wanakumbushwa kutokubali kuburuzwa na baadhi ya wanaume wenye tabia ya uongo.

Unaanzaje kumsaliti mpenzi wako? Unakubalije uongo wa mtu mpaka unakubali kumuacha mumeo kwa ajili yake, huku ukienda sehemu ambayo ni kama kucheza kamari?

Hebu fuateni maneno ya Kikwete, kuwa," akili za kuambiwa changanya na zako." Mtu anakwambia atakujengea nyumba, atakununulia gari, TV ya kisasa, friji, wakati hata ukimwangalia wakati mwingine hafanani na hivyo.

Wanaume wa aina hii hawajaanza jana, leo wala hawataisha. Ndiyo maana hata huko nyuma, wanamuziki walitunga na kuimba nyimbo za kutahadharisha.

Orchestra Safari Sound (OSS) katikati ya miaka ya 1980, ilifyatua kibao kiitwacho 'Homa Imenizidia', kilichotungwa na Hassan Bitchuka, kinachomzungumzia mwanamama mmoja aliyelaghaiwa na mwanaume amwache mumewe, lakini baada ya jamaa kupata anachokitaka, akamwacha kwenye mataa. Mwanamama sasa analalamika na kuwaasa wenzake.

"Homa imenizidia miye ho, kutwa nashinda nalia, jua linapochomoza, machozi mie hunitoka. Visa alivyonitenda Rehani oo, sitovisahau kamwe, amenishawishi nimuache mume wangu, ili niishe naye. Nimeachwa na mume wangu, nimekwenda kwa Rehani oo, baada ya muda si mrefu, kasema niondoke eti sina tabia nzuri ooo.

Mamaaa, yamenikuta, mamaaa, yamenikuta

ndugu zangu mlioolewa, mjihadhari na wadanganyifu, mkiachana na waume zenu mtapotea ooo. Nimesimama katikati ya njia panda, jua linazidi kuzama mama, mama, mama ooo Mamaaa, yamenikuta, mamaaa, yamenikuta."

Siku zote kinamama na kinadada wakumbuke kuwa mwanamume anayekudanganya umwache mpenzi wako au mumeo na ukamfuata yeye, anakuwa na wasiwasi kuwa iko siku na yeye yatamkumba. Ndiyo maana akitimiza haja zake anakuacha.

Bendi ya Magereza Jazz mwanzoni mwa miaka ya 1990, ilitoa kibao maarufu kiitwacho 'Ashura.' Kinazungumzia dada anayewaasa wenzake wasiachane na waume zao kwani yatawafika makubwa baada ya yeye mwenyewe kumpata yaliyompata.

"Ashura mimi najuta, mwenzenu kweli najuta sasa, visa navyofanyiwa na bwana huyu, nimeamini methali isemwayo, mkataa pema, pabaya panamwita.

Leo hii mwenzenu kusema hivi mimi, nina maana yangu, nimedanganyika, kumuacha mume wangu, kumfuata bwana mwenyewe, kumbe ni muongo kweli, kumbe hasidi.

Visa navyofanyiwa na bwana huyu, nimeamini methali isemwayo, mkataa pema, pabaya panamwita.

"Leo hii mwenzenu kusema hivi mimi, nina maana yangu, nimedanganyika. Kumuacha mume wangu, kumfuata bwana mwenyewe, kumbe mwizi baba kweli, kumbe ni muongo. Nawahusia wanawake wenzangu wote heheheee, mziheshimu ndoa zenu zisije vunjika. Mjiepushe na mabwana wadanganyifu Ashura, anakupenda wakati una mumeo oohooo, ukishaachika wala hana habari nawe.

"Keshakudanganya kwa 'curly' na 'relaxer', keshakudanganya kwa vitenge vya Zaire, keshakudanganya kwa cheni za dhahabu, keshakudanganya kwa pesa na mabasi, na starehe za muda hazina mwisho Ashura. Nawahusia wanawake wenzangu wote heheheee, mziheshimu ndoa zenu zisije vunjika.

"Mjiepushe na mabwana wadanganyifu eee mama, anakupenda wakati una mumeo oohooo, ukishaachika wala hana habari nawe, keshakudanganya kwa chipsi na mayai, keshakudanganya kwa bia na ma-kuku, keshakudanganya kwa khanga za Mombasa, keshakudanganya kwa ngoma za mkote, na starehe za muda hazina mwisho sikia."

Mwenye masikio ya kusikia na asikie.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya sumu-2

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WE bibie, mbona unakata wakati mwenzako sijamaliza? Yamekuingia ee, pole sana. Sasa nachokwambia ni hiki, hivi sasa huyo bwana unayeringia ninaye miye. Usishangae, ninaye hapa ndani hivi navyokueleza, najua anaoga nini, anakula nini, na anavaa vipi, ulidhani ukiolewa bwana atakuwa wa kwako peke yako ee, huyu hapa dada. Au nikupe simu uongee naye, hahahaha, utakufa kwa presha bure sikupi. Yaani umeolewa lakini bwana kaja kwangu, loh! Mwanamke gani usiyejua kumlea mwanaume, mwanamke usiyejua kumnyeyekea bwana, mwanamke usiyejua mahaba, tena ninavyokwambia bwana ninaye miye, bwana yumo ndani anajilia vyake...” Husna akakata tena. mambo yalikuwa yamemzidi sasa. Akatamani aibamize simu ukutani, lakini nguvu hakuwa nazo mikononi. Akawa anatetemeka mwili mzima. Akalia zaidi ya mwanzo. Safari hii aliona huenda kinachoongewa hata kina asilimia kubwa ya ukweli.

Ni wiki mbili sasa tangu alipoagana na mumewe ambaye alimuaga kuwa anakwenda Zanzibar kikazi. Na amekuwa akiwasiliana naye kila siku, akiongea naye, akimpa moyo na matumaini kuwa baada ya wiki mbili tu atarejea nyumbani wafurahi pamoja.

“Kumbe yuko kwa hawara zake!” Akajikuta akiongea kwa sauti kubwa ya ukali “Sasa kwa nini ulinitoa kwetu, kwa mama yangu kuja kuniweka kwenye hatari hii Dan? Unawapa namba hawara zako wanitukane?” Akamuuliza mumewe ambaye hayupo. “Ngoja arudi atanitambua!”

************************************

Hakupata hata tone la usingizi. Alikuwa akiwaza na kuwazua. Ndoa yake changa, lakini tayari aliiona ni kama imeingia na mdudu nuksi. Na kwa bahati mbaya sana hakuwa na uzoefu na kitu kama hicho. Ilimuumiza sana. Akaanza kukumbuka aliwahi kuwasikia zamani akinamama wakisema ndoa si kitu cha mchezo. Yataka moyo. Ndoa ina tamu na chungu. Pamoja na yote, kwake yeye anaona kama chungu inaanza mapema sana kabla tamu yaijakolea.

Kwa sababu hakuwa na usingizi aligaragara tu kitandani. Mara ageukie huku mara kule. Mawazo tele kichwani.

Mawazo yakamrudisha nyuma wiki mbili zilizopita wakati mumewe akijiandaa kuondoka. Waliongea vizuri. Walikuwa kwenye kilele cha furaha na hata hawakupika nyumbani. Badala yake walinunua na kula chips na kuku.




**“Hivi dada unajifanya umeolewa eee! Wewe ni mlinda nyumba tu. Mimi mwenzako hata ndugu zake wananifahamu hadi leo hii. Mimi ndiyo wanenitambua kuwa wifi yao na shemeji yao, wewe umekaa hapo kama boya tu.”**

Akakumbuka asubuhi alipoamka mapema na kupika chai ya maziwa, na akakaanga mayai yaliyokuwa na slesi za mikate wakati wa kifungua kinywa. Ilikuwa ni furaha na amani tele.

Akachota maji, na baada ya hapo akaenda sokoni kununua kitoweo, akapitia kwa fundi kupeleka simu yake iliyokuwa imeharibika spika. Akarejea nyumbani.

Akakumbuka mchana alimsindikiza mumewe hadi kwenye stendi ya Mabibo, alipopanda daladala akarejea nyumbani. Hakumsindikiza hadi Forodhani ambako hupandia boti kwenda Zanzibar.

Hii ilimfanya kufikiria kuwa huenda hakwenda Zanzibar, yupo hapa hapa Bara kwenye moja kati ya nyumba za wageni au hawara yake aliyepiga simu.

Akafikiria kuwa huenda mwanamke huyo alikuwa amemtafuta muda mrefu, kwani alikaa wiki nzima hajakwenda kuchukua simu yake kutokana na ukosefu wa pesa.

Alikuwa akisubiria pesa yake ya upatu ndiyo akaichukue. Na kweli leo alipokwenda kuichukua, ile kuifungua tu, hata haikupita dakika 10, simu ya kwanza ni ya mwanamke huyo hasidi.

Aliinuka kitandani mapema zaidi kuliko kawaida yake. Akaanza kufanya kazi zake kivivuvivu. Mwili ulikuwa ukifanya kazi, lakini akili bado ilikuwa ikimuwaza mumewe na huyo mwanamke.

Kila akitaka kumpigia mumewe moyo unakataa. Aliona hawatoongea kwa amani. Wataongea kwa shari na hakutaka sauti yake ipae majirani wasikie, kwani si tu kwamba hakutaka kuonekana anagombana na mumewe, lakini aliona aibu kwa majirani wenzake wasikie wana ugomvi ikiwa ni miezi michache tu baada ya kufunga ndoa. Hilo jambo halikumpendeza hata kidogo. Akavuta subira Dan arejee ili ajue nini la kufanya.

Kwa muda mrefu sana hakuifungua simu yake. Ni mtu mmoja tu aliyemuogopa. Ni yule dada asiyemfahamu. Akaona aiwashe kwanza, kwani anaweza kupigiwa na mumewe, lau hata amuongopee. Yeye mwenyewe hakutaka kabisa kumpigia.

Sekunde chache tu baada ya kuifungua meseji moja ikaingia. Kabla hajafanya chochote, akaifungua. Akauma meno. Akafumba macho. Akayafumbua. Akaiangalia meseji ile. Ndiyo ilitoka kwa yule yule. Akaisoma. Alipoimaliza, akaamua kitu kimoja.

Akaizima simu hiyo. Akaapa hatoitumia tena. Kwa sababu anaonekana anaandamwa sana na huyo dada hawara ya mumewe.

“Kama ni hivi, sitoitumia tena simu hii. Yaani kaninunulia simu ili niwe natukanwa na hawara zake? Siitaki tena. Siitaki simu wala laini. Sitaki kujipa presha nife bado kijana mtoto wa watu. Pesa ya upatu bado ninayo nitakwenda kununua kiswaswadu changu, nitakwenda kusajili laini yangu ya kampuni nyingine ya simu ili niondokane na mateso haya. Sitosikia tena manyanyaso, kejeli, dharau na vitisho na Dan kama ataipata hii namba, sijui! Akawape tena hawara zake! Haiwezekani!

“Hivi dada unajifanya umeolewa eee! Wewe ni mlinda nyumba tu. Mimi mwenzako hata ndugu zake wananifahamu hadi leo hii. Mimi ndiyo wananitambua kuwa wifi yao na shemeji yao, wewe umekaa hapo kama boya tu.” Haya ndiyo maneno yaliyoandikwa kwenye hiyo meseji.

Alitaka kupotezea, lakini donge lilimkaa rohoni hata mate yalishindwa kupita. Akaona hapana. Majira ya mchana, akiwa na dera lake lililochakaa na kupauka ambalo mara nyingi hushinda nalo nyumbani, akavaa kandambili ambazo huenda nazo bafuni. Hakuwa na haja ya kupaka walau mafuta au kuweka nywele vizuri. Khanga moja alijifunga kiunoni, moja akiishika mkononi pamoja na mtandio wake ambao hata hakujisumbua kuuwekwa kichwani, badala yake akatundika begani. Huyo akaanza kukata mitaa kuelekea anakoelekea. Njiani alionekana kama chizi. Kila aliyemuona alishangaa. Alionekana anaongea peke yake. “Ameshavurugwa.” Baadhi ya watu waliambizana njiani.

“Kumbe wanalijua hili, watanitambua.” Mabibo na Manzese Tip Top sio mbali sana. Huko ndiko ukweni kwa Husna.

Wakwe halisi baba na mama Dan wote walishafariki kabla ya hata hajaolewa. Waliobaki ni wifi na shemeji zake tu ambao walikuwa wanaishi kwenye nyumba za urithi wa wazazi wao.

Alifika Tip Top kwa kudra za Mwenyezi Mungu tu, kwani alipishana na watu, bodaboda, magari, mikokoteni, maguta wakati mwingine yeye mwenyewe akiwa hajui hata anapishana na nini. Akili yake haikuwepo alipo. Alikuwa akifikiria mengi yaliyomfanya awe kama kichaa.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# STEVE NYERERE AMCHARUKIA ZUMARIDI

MWIGIZAJI na mchekeshaji Steve Nyerere, amemcharukia Mfalme Zumaridi, kuwa anapotosha watu na kama angekua na wadhifa serikalini angemchukulia hatua.

Amesema mchungaji huyo anaposema ameonana na Mungu ni jambo zito na ni upotoshaji.

"Lazima aheshimu imani ya dini, kuchezea na hisia za watu kiimani ni jambo baya, lazima aachane na mambo haya, ningekuwa kiongozi wa serikali ningemfunga jela," amesema Nyerere.



## Chameleon, Bobi Wine hawali sahani moja

MSANII mkongwe wa muziki nchini Uganda, Jose Chameleone, amekiri kuwa na ugomvi na kiongozi wa upinzani Bobi Wine.

Chameleone akizungumza na vyombo vya habari hivi karibuni, amesema alikuwa anamheshimu mwanasiasa huyo na pia mwanamuziki hata kipindi alipojeruhiwa wakati wa rabsha za siasa alilia kwa uchungu.

Lakini alikuja kumchukia wakati shoo yake ya Gwanga Mujje ilipovunjwa, Bobi Wine alikuwa mmoja wa watu waliomcheka.

"Wakati jukwaa langu lilipoanguka, niliona marafiki ambao walikuja kunipa pole na wale walionicheka," alisema Chameleone.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMWINDA KANE

REAL Madrid inafuatilia yanayoendelea na mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake na Spurs unamalizika ifikapo mwaka 2024 na amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kuhamia Manchester United au Bayern Munich. (***Mail***)

### CITY YAMBANA HAALAND

KIPENGELE cha kuachiwa cha euro milioni 200 kilichoandikwa katika mkataba wa Erling Haaland na Manchester City si halali tena na klabu hiyo itaweza kuweka bei yao wenyewe iwapo itataka kumuuza mshambuliaji huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2027. (***Goal***)

### MITOMA, BRIGHTON SAFI

KLABU ya Brighton iko tayari kumpa winga wa Timu ya Taifa ya Japan, Kaoru Mitoma, mwenye umri wa miaka 25, mkataba utakaoweka rekodi huku Real Madrid, Manchester City na Arsenal wakionyesha nia yao. (***Goal***)

### UPOLE WAMPONZA VIEIRA

PATRICK Vieira alitimuliwa kama kocha wa Crystal Palace kwa sababu iliaminika alikuwa mpole sana kwa wachezaji wake. (***Mirror***)

### RICE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA imeonyesha "nia na shauku ya juu" kumsajili mchezaji wa West Ham, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24 kwa ajili ya msimu ujao. (***Florian Plettenberg***)

### KANTE KUBAKIA CHELSEA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa anayesumbuliwa na majeraha, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 31 ambaye hajacheza tangu Agosti, mwaka jana kwa sababu ya tatizo la misuli ya paja lakini anaendelea kurejea katika hali nzuri - "yuko tayari" kusaini mkataba mpya wa miaka miwili Chelsea. (***Sun***)

### DE JONG ANOGEWA BARCA

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, ambaye amekuwa akilengwa kwa muda mrefu na Manchester United na Chelsea, alisema katika mahojiano kwenye televisheni ya Hispania: "Barca imekuwa klabu ya ndoto zangu siku zote... natumaini kuendelea kuwa hapa kwa miaka mingine mingi".(***TV3***)

### IWOBI BADO AJIPANGA

KIUNGO wa kati wa Nigeria, Alex Iwobi, mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake wa sasa na Everton unaendelea hadi msimu wa 2024, amepewa mkataba mpya, lakini anasubiri kuona jinsi msimu utakavyoisha kabla ya kuusaini. (***Football Insider***)

### CHAMBERLAIN NJIA MOJA

LIVERPOOL itamruhusu kiungo wa kati wa zamani wa England, Alex Oxlade-Chamberlain, mwenye umri wa miaka 29 na Naby Keita (28) kuondoka kama wachezaji huru katika msimu ujao. (***Athletic***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BABA AKANUSHA UVUMI MESSI KUONDOKA PSG

## ● ● ● Asema bado klabu pamoja na mchezaji huyo wa Argentina wako katika…

**PARIS,** Ufaransa

BABA wa Lionel Messi, Jorge amedai "habari za uongo" zinaenezwa kuhusu mustakabali wa nyota huyo katika klabu ya Paris Saint-Germain.

**Mchezaji wa kimataifa wa Argentina, Messi anatarajiwa kumaliza mkataba wake na Parc des Princes mwishoni mwa msimu huu, jambo ambalo linazidisha mazungumzo kuhusu uhamisho wake ujao wa soka.**

Ripoti ya wiki hii ilisema PSG haiko tayari kukubali malipo ya Messi kuhusu mkataba mpya, huku nyingine ikidai kuwa ofa imetolewa ya euro milioni 600 ili kujiunga na Al Hilal ya Saudi Arabia.

Pia ilidaiwa Ijumaa Messi aliondoka kwenye mazoezi mapema wiki hii kutokana na kutofautiana na kocha mkuu, Christophe Galtier.

Hata hivyo, Jorge Messi amekanusha taarifa hizo.

"Utaachwa lini uongo?" aliandika kwenye akaunti yake ya Instagram.

"Ushahidi uko wapi? Lo, yote ni ya uongo. Sawa. Haijalishi. Usiamini. Hatutavumilia tena habari za uongo."

Messi ana mabao 18 na asisti 17 katika mechi 31 alizochezea PSG msimu huu, lakini alikosolewa kwa kuonyesha kiwango kibovu wakati PSG ikiondolewa katika hatua ya 16 bora ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wa mshindi huyo wa Kombe la Dunia katika mkutano na waandishi wa habari siku ya Ijumaa, Galtier alisema: "Ninajua Leo Messi na bodi wamekuwa katika mazungumzo.

"Kuhusu kama Leo Messi atakuwa hapa msimu ujao au la, siwezi kusema. Najua watu wanajadili hilo, lakini Leo Messi ana furaha kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Ana mabao 18 na asisti 17 msimu huu. Najua kulikuwa na ukosoaji kuhusu mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich, lakini hakuwa peke yake.

"Kuhusu mustakabali wake, ni mapema mno kujua kitakachotokea."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
REAL MADRID
1 | 2.20
X | 3.30
2 | 3.01

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# PEDRI KUIKOSA EL CLASICO

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Barcelona, Pedri atakosa mechi dhidi ya Real Madrid maarufu El Clasico itakayochezwa leo kutokana na tatizo la misuli ya paja.

Vyanzo vimeiambia ESPN licha ya kufanya mazoezi akiwa na Hispania pamoja na wachezaji wenzake hapo juzi, nyota huyo hayuko sawa kwa mchezo huo mkubwa pale Camp Nou.

Pedri amekuwa nje ya uwanja tangu apate jeraha la mguu wake wa kulia katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi ya Europa iliyochezwa Februari 16, mwaka huu.

Kocha wa Barca, Xavi alikuwa na matumaini na Pedri lakini baada ya kikao cha Ijumaa, mchezaji huyo hakujisikia kuwa tayari na hataharakishwa kurudi.

Pedri pia hatacheza mechi zijazo za Hispania za kufuzu kwa euro 2024 dhidi ya Norway na Scotland.

Barca itaingia kwenye mchezo huo wa ligi ikiwa pointi tisa mbele ya wapinzani wao Real Madrid zikiwa zimesalia mechi 13.

# Vieira atimuliwa Crystal Palace

**LONDON,** England

PATRICK Vieira ametimuliwa kuwa kocha wa Crystal Palace baada ya mwenendo mbaya ambao umeifanya timu hiyo kukosa ushindi katika mechi 12 zilizopita, taarifa rasmi ya klabu hiyo imetangaza.

Vieira alijiunga na klabu hiyo mwaka wa 2021 na kuiongoza kumaliza katika nafasi ya 12 msimu uliopita.

Palace sasa wako katika nafasi ya 12 kwenye Ligi Kuu England, lakini wako pointi tatu tu juu ya eneo la kushushwa daraja.

Mwenyekiti wa Palace, Steve Parish, alisema katika taarifa yake: "Ni kwa masikitiko makubwa uamuzi huu mgumu umefanywa.

"Hatimaye, matokeo ya miezi ya hivi karibuni yametuweka katika hali mbaya ya ligi na tuliona mabadiliko ni muhimu ili kutupa nafasi nzuri zaidi kubakiza hadhi ya Ligi Kuu.

Palace pia ilisema Vieira, Osian Roberts, Kristian Wilson na Said Aigoun, wameondoka katika benchi la ufundi la klabu hiyo.



CHEZA USHINDE KASINO

# JOTO LA SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS LAANZA

**Na Saada Akida**

ZIKIWA zimebakia siku tatu kabla watani wa jadi, Simba Queens kuvaana na Yanga Princess, makocha wa timu hizo kila mmoja ametamba timu yake imeimarika na itaibuka na ushindi katika mchezo huo wa marudiano wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Yanga Princess ndio mwenyeji wa mchezo huo utakaochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Yanga ikitangulia kupata bao na mabingwa watetezi, Simba walisawazisha kupitia Viviane Corazone.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Sebastian Nkoma, alisema wanaendelea kufanya maandalizi ya kuelekea mchezo huo na anaamini kikosi chake kitawasimamisha vinara yao wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini.

Nkoma alisema kikosi cha kipo imara baada ya kufanyia kazi madhaifu waliyokuwa nayo na waliyoyaonyesha katika mechi iliyopita waliyocheza ugenini dhidi ya Mkwawa Queens.

"Tunafahamu mechi ya kwanza tulitoka sare, kipindi hicho timu ilikuwa ndio inaanza, hatukuwa na muunganiko mzuri, lakini hii mechi ya mzunguko wa pili tuko vizuri na tunatarajia kufanya vizuri, naamini tutavuna matokeo bora," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa Jumatano ni kati ya Baobab Queens dhidi ya JKT Queens, Amani Queens itawavaa Ceasiaa Queens kwenye dimba la Ilulu, Lindi na Mkwawa Queens watawaalika Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Samora wakati Alliance Girls itakuwa uwanjani dhidi ya The Tigers Queens kutoka Arusha.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pindi Chana (kulia), akimpongeza mchezaji bora wa kike kwa upande wa mchezo wa tenisi kwa watu wenye ulemavu, Rehema Said, baada ya kushinda tuzo hiyo kwa mwaka 2022 iliyotolewa na serikali kupitia Baraza la Michezo la Tanzania (BMT). **PICHA: SAADA AKIDA**

# Vichapo vyatawala RCL 2023

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya Mabingwa wa Mikoa (RCL), imeendelea katika vituo vinne vya Katavi, Kagera, Shinyanga na Kigoma, huku baadhi ya timu zikitoa vipigo vitakatifu kwa wapinzani wao.

Buhaya FC ambayo hivi karibuni ilitolewa kwenye michuano ya Kombe la FA, inaonekana imepata uzoefu kwa kupata ushindi mnono wa mabao 10-0 dhidi ya Damali FC ya Simiyu, Mapinduzi ya Mwanza ikiisasambia Geita Academy magoli 7-0.

Kituo cha Kigoma zinapochezwa mechi za Kundi B, Mambali Ushirikiano ya Tabora ilikiona cha moto, ilipochabangwa mabao 3-2 na Kilosa United ya Morogoro, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, katika mechi ya mapema, na baadaye Tanesco Kilimanjaro walichapwa mabao 2-0 dhidi ya Aglo Sports Academy ya Kigoma.

Buhaya ndio vinara katika Kundi A ikiwa na pointi 10 wakati Kundi B linaongozwa na Arusha City yenye pointi saba kwa mechi tatu ilizocheza, ikifuatiwa na Singida Cluster, Anuary FC ya Shinyanga ikiliongoza Kundi C ikiwa na pointi tisa.

Tanzania Navy ya Dar es Salaam iko katika nafasi ya pili kwa zikitofautiana mabao kwenye Kundi B linaongozwa na Malimao FC ambayo imeshinda mechi zote tatu, ikiwa na pointi tisa, ikifuatiwa na Ilula Tigers ya Iringa yenye pointi sita.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 19/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5460 | FK Khimki vs Rostov | 3.24 | 3.39 | 2.06 |
| 14:15 | 4378 | Groningen vs Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 14:30 | 3192 | Sampdoria vs Verona | 2.85 | 3.00 | 2.46 |
| 15:00 | 1475 | AC Ajaccio vs Monaco | 4.70 | 3.50 | 1.69 |
| 15:00 | 5011 | Sheffield Utd vs Blackburn | 1.64 | 3.64 | 4.79 |
| 15:00 | 5161 | Kolos Kovalivka vs FC Minaj | 1.97 | 3.02 | 3.69 |
| 15:30 | 5723 | Swansea vs Bristol City | 2.09 | 3.25 | 3.30 |
| 16:00 | 3678 | Betis vs Mallorca | 1.80 | 3.15 | 4.60 |
| 16:00 | 5924 | Shakhtar Donetsk vs Rukh Vinnyky | 1.19 | 5.54 | 11.28 |
| 16:30 | 4013 | SBV Excelsior vs Cambuur | 2.56 | 3.32 | 2.51 |
| 16:30 | 5813 | Ajax vs Feyenoord | 1.71 | 3.92 | 4.02 |
| 17:00 | 1276 | Torino vs Napoli | 4.23 | 3.32 | 1.81 |
| 17:00 | 1452 | Troyes vs Brest | 2.75 | 3.20 | 2.41 |
| 17:00 | 1649 | Nice vs Lorient | 1.63 | 3.71 | 4.81 |
| 17:00 | 2211 | Fiorentina vs Lecce | 1.58 | 3.69 | 5.39 |
| 17:00 | 2358 | Aalborg vs Randers | 2.40 | 3.44 | 2.73 |
| 17:00 | 3788 | Silkeborg vs Midtjylland | 2.23 | 3.65 | 2.84 |
| 17:00 | 3814 | Strasbourg vs AJ Auxerre | 1.95 | 3.26 | 3.71 |
| 17:00 | 4291 | Istra vs Lokomotiva Zagreb | 2.46 | 3.10 | 2.63 |
| 17:00 | 5361 | Montpellier vs Clermont Foot | 1.83 | 3.35 | 4.10 |
| 17:00 | 5512 | Copenhagen vs Viborg FF | 1.43 | 4.45 | 6.68 |
| 17:00 | 5730 | Arsenal vs Crystal Palace | 1.27 | 4.88 | 9.95 |
| 17:00 | 5748 | Zeljeznicar vs FK Sloga Doboj | 1.59 | 3.52 | 5.39 |
| 17:00 | 5964 | Lyngby vs Horsens | 2.02 | 3.44 | 3.44 |
| 17:15 | 5608 | Brighton vs Grimsby | 1.10 | 7.95 | 15.90 |
| 17:30 | 2629 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.34 | 3.10 | 2.95 |
| 18:15 | 1499 | Osasuna vs Villarreal | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 18:15 | 3458 | Real Sociedad vs Elche | 1.36 | 4.39 | 7.98 |
| 18:30 | 4002 | BSC Young Boys vs FC Basel | 1.73 | 3.78 | 4.10 |
| 18:45 | 4336 | Vitesse Arnhem vs PSV Eindhoven | 4.31 | 3.91 | 1.66 |
| 19:00 | 1168 | Austria Vienna vs Rapid Vienna | 2.47 | 3.24 | 2.52 |
| 19:00 | 3118 | RB Salzburg vs SCR Altach | 1.14 | 6.58 | 12.33 |
| 19:00 | 5521 | Tromso vs Lillestrom | 2.79 | 3.15 | 2.36 |
| 19:05 | 4170 | Paris St Germain vs Rennes | 1.46 | 4.42 | 5.63 |
| 19:30 | 3282 | Manchester Utd vs Fulham | 1.47 | 4.11 | 5.80 |
| 19:30 | 3669 | Bayer Leverkusen vs Bayern Munchen | 4.46 | 4.18 | 1.60 |
| 19:30 | 4171 | Dinamo Zagreb vs HNK Rijeka | 1.36 | 4.32 | 7.00 |
| 19:30 | 4816 | CSKA Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.29 | 3.34 | 2.06 |
| 20:00 | 1639 | Viktoria Plzen vs Bohemians | 1.46 | 4.42 | 5.89 |
| 20:00 | 5119 | Lazio vs Roma | 2.66 | 2.91 | 2.71 |
| 20:30 | 4962 | Getafe vs Sevilla FC | 2.82 | 2.97 | 2.51 |
| 21:00 | 3255 | Sporting Braga vs Porto | 3.08 | 3.28 | 2.20 |
| 21:15 | 3393 | KAA Gent vs Eupen | 1.35 | 4.82 | 7.43 |
| 21:30 | 2698 | Mainz vs SC Freiburg | 2.10 | 3.36 | 3.16 |
| 22:00 | 5465 | Twente vs AZ Alkmaar | 2.15 | 3.31 | 3.11 |
| 22:30 | 4292 | AEK Athens vs Panathinaikos | 1.75 | 3.23 | 5.19 |
| 22:45 | 1105 | Inter vs Juventus | 1.92 | 3.30 | 3.75 |
| 22:45 | 4187 | Reims vs Marseille | 2.79 | 3.29 | 2.33 |
| 23:00 | 5791 | Barcelona vs Real Madrid | 2.20 | 3.30 | 3.01 |
| 23:30 | 1399 | Boavista vs Famalicao | 2.31 | 3.17 | 2.97 |

# Michezo

Nipashe

Jumapili Machi 19, 2023



Vieira atimuliwa Crystal Palace

# Simba yafanya mauaji Afrika

**Na Adam Fungamwango**

THIS is Simba. Mnyama ametinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 7-0 dhidi ya Horoya AC kutoka Guinea katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana.

Kiungo mshambuliaji Mzambia Clatous Chama ndiye aliyeongoza mauaji hayo akifunga mabao matatu 'hat-trick', straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jean Balake na Saido Kanoute raia wa Mali wakifunga mabao mawili kila mmoja.

Unakuwa ni ushindi mkubwa zaidi katika michuano hiyo hatua ya makundi, na inakuwa ni mara ya nne kwa Simba kutinga hatua ya robo fainali ndani ya miaka mitano, mara tatu ikiwa Ligi ya Mabingwa Afrika na mara moja Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa matokeo ya jana, Raja Casablanca ya Morocco na Simba ndizo zilizofanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo kutoka Kundi C, licha ya 'Waarabu' hao kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Vipers, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa St Marys Chitende ulioko Entebbe, Uganda.

Horoya ndiyo walioanza kulifikia lango la Simba dakika ya saba ya mchezo, kupitia kwa yule yule aliyewaliza Februari 11, mwaka huu huko Guinea, Pape N'Diaye alipoupata mpira uliokuwa umeokolewa vibaya na mabeki, akapiga shuti ambalo lilitoka nje kidogo ya lango.

Dakika ya tisa, Simba iliandika bao kupitia kwa Chama kwa mkwaju wa faulo baada ya Mkongomani, Jean Baleke kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari, ambapo Chama alipiga shuti kali la mguu wa kulia lililowapita juu mabeki waliokuwa wamejipanga, ukakatika kulia kwa kipa Mohamed Kamara ukajaa wavuni licha ya juhudi zake za kuchupa kutaka kuuokoa.

Alikuwa ni Chama aliyeupata mpira katikati ya uwanja baada ya kukosewa na wachezaji wa Horoya, akakimbia nao umbali mrefu na kuingia ndani ya eneo la hatari, akimuondoa kipa Makara langoni kumfuata, akaupiga pembeni kwa wachezaji wao wawili, lakini wote wakashindwa kuukwamisha wavuni.

Baleke aliukwamisha wavuni mpira, akiipatia Simba bao la pili dakika ya 32, akimalizia mpira uliotemwa na kipa Kamara.

Pasi safi ya Ntibazonkiza, ilimkuta Kibu ambaye aliachia shuti kali lililotemwa na kipa Kamara, kabla ya kumkuta mfungaji.

Dakika tatu baadaye Chama aliukwamisha mpira wavuni kwa mkwaju wa penalti, baada ya beki mmoja wa Horoya kuunawa mpira uliopigwa na Kapombe.

Kipindi cha pili timu zote ziliendelea kufunguka na kushambuliana kwa zamu, na dakika ya 55, Sadio Kanoute alifunga bao la nne kwa shuti kali, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Saido na Kapombe.

Baleke alifunga bao la tano dakika ya 66, lililotokana na kumnyang'anya mpira beki mmoja wa Horoya na kwenda kuukwamisha wavuni akimhadaa kipa Sekou Sylla aliyeingia badala ya Kamara.

Chama alikamilisha 'hat-trick' yake, ikiwa ni bao la sita kwenye mchezo huo dakika ya 70, ulioanzia kwa Pape Sakho aliyetokea benchini, akampa Saido ambaye alipiga krosi kwa mfungaji, kabla ya kuukwamisha wavuni aliwahadaa na kuwagaragaza kwa chenga kipa na walinzi wake.

Kanoute alipigilia msumari kwenye jeneza la Horoya dakika ya tatu kabla ya mechi kumalizika baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Moses Phiri na Kapombe, kabla ya kumpa mfungaji aliyeumisha wavuni kwa staili ile ile ya bao lake la kwanza na la nne kwa shuti kali la mbali.

Simba pia imevuna kiasi cha Sh. milioni 35 kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutokana na kufunga mabao saba.

### ●●● Yatinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kibabe, Chama akipiga...



Wachezaji wa Simba, Aishi Manula (kushoto), Sadio Kanoute (katikati) na Henock Inonga, wakishangilia bao katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana usiku. Simba ilipata ushindi wa mabao 7-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga : Waje Tuwamalize

**Na Saada Akida**

FULL shangwe ndio kauli mbiu rasmi inayotumiwa na klabu ya Yanga katika mbio za kusaka tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika huku leo ikiwakaribisha US Monastir kutoka Tunisia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga yenye pointi saba inahitaji ushindi ili kukamilisha hesabu zake za kusonga mbele katika michuano hiyo kwa kuwafuta US Monastir wenye pointi 12.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema mechi hiyo ni muhimu kwa sababu wakipata matokeo mazuri watakuwa wamefuzu hatua ya robo fainali huku wapinzani wao wakicheza bila presha.

Nabi alisema US Monastir imekuja kutafuta matokeo chanya na sio kutalii, hivyo anafahamu mchezo huo utakuwa na ushindani wa kila upande kupambana kupata matokeo mazuri ambayo yatawaimarisha kwenye msimamo wa kundi lao.



Alisema kurejea kikosini kwa nyota wao wawili, Fiston Mayele na Kennedy Musonda, ni faraja na kunaongeza nguvu ya timu yao kuelekea mchezo huo wa kufa au kupona.

Naye Kocha Mkuu wa US Monastir, Darko Novic, alisema wamejiandaa kufanya vizuri kwa sababu tayari wamefuzu robo fainali ya michuano hiyo, watacheza bila presha na lengo lao ni kuweka rekodi ya kumaliza hatua ya makundi bila kupoteza.

"Maandalizi hayakuwa magumu sana, kwa sababu tunawajua Yanga, tumekuja kukamilisha ratiba, maeneo yote katika kikosi changu tumefanyia mazoezi, hatutokubali kupoteza mchezo huu," alisema Novic.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >